Kiwango Cha Sasa Cha Huduma Yangu

. . . ufufuo, nikiwa nimechoka sana na kudhoofika. Nasi tumekuwa na ushirika mwingi sana njiani, mikutano ya ajabu, pamoja na salamu za Wakristo huku na huko, toka huku na huko katika Pwani ya Mashariki, na pia kule Pwani ya Magharibi hadi Canada. Na pamoja na ushirikiano mzuri kati ya makanisa yote mbali mbali ya kidhehebu, ya Assemblies of God na United Pentecostal, Church of God, Foursquare, na mengi ya madhehebu ambayo yalishirikiana tukawa na mikutano mikubwa. Mafanikio makuu, vile yawezavyo kuitwa mafanikio siku hizi, na labda wengi wangeyaita "makuu." Lakini mimi binafsi, mi—mi—mimi ni mwana ufufuo. Na ufufuo, nikinena kitaifa karibu tu umekwisha. Na sisi tuko . . . Napenda kuona ufufuo ambapo mioyo inawashwa, si kuongeza washirika, bali ufufuo. Bwana wetu alifanya miujiza mingi ya kuwaponya watu, na, hakika, baadhi yao waliokoka. Na sasa niko nyumbani, nikipumzika kwa muda mchache, na nitarudi kazini katika majuma machache, Bwana akipenda.

2 Na sasa hili ni kwa watu wengi na marafiki zangu kote duniani. Nataka kusema usiku huu, hapa Maskanini, ikiwa wewe, ye yote wenu angekuwako na angeona, wao wana joto sana Maskanini usiku huu. Watu wamejazana ndani, wamesimama milangoni, na nje katika magari na kwingineko, na kuna joto sana, itakuwa vigumu kwa watu na kwangu pia.

3 Lakini nimekuja mahali hapa kwa sababu nataka kueleza ni kiwango gani cha wakati tunaoishi kulingana na huduma ambayo Bwana alinipa. Nami nilitaka unasiwe humu Maskanini. Ulikuja moyoni mwangu majira ya katikati ya mwaka, lakini nilingoja hadi nirudi humu ili ni—nipate kuunasa, niwatumie enyi watu wa duniani.

4 Imekuwa miaka thelathini na miwili iliyopita, ambapo Bwana Yesu, yapata umbali wa yadi mia na hamsini toka ninaposimama hivi sasa, hapa Jeffersonville kwenye Barabara ya Nane na ya Penn, asubuhi nilipoweka jiwe la pembeni kwenye Maskani haya, pakiwa tu bwawa la matope. Nami niliishi ng'ambo ile nyingine upande wangu wa kushoto hapa. Ilikuwa kabla sijaoa. Nilikuwa ninaishi na baba na mama yangu. Basi Bwana Yesu aliniamsha asubuhi ambayo jiwe la pembeni lingewekwa; karibu mapema, kama saa kumi na mbili alfajiri. Nami nilikuwa nikilala kitandani kwa muda, huku moyo wangu umejaa furaha, nikiwaza kuhusu wakati huu mkuu ambapo

Bwana Mungu angenipa maskani ya kuhubiria. Kwa wakati huo nilikuwa tu mvulana kijana. Na siku hiyo nili . . . yule msichana niliyekuwa nikienda naye, ambaye punde angekuwa mke wangu mwaka uliofuata, angekuwa pamoja nasi siku hiyo kuweka jiwe la pembeni.

5 Nami nakumbuka asubuhi hiyo nilipokuwa nimeamka, nikalala chumbani, orofani papa hapa karibu na Barabara ya Saba. Kitu fulani kilisema, "Amka usimame." Nami nikasimama. Na niliona, kama ilivyokuwa, mahali pakuu, na ilikuwa kama ma—ma—mahali ambapo mto ulipitia bondeni. Nami nilikwenda chini huko mtoni na nikafahamu kuwa ni mahali ambapo Yohana Mbatizaji alikuwa akiwabatizia watu, nao walikuwa wamepageuza kuwa zizi la nguruwe. Nami nilipinga jambo hilo sana, nikisema tu hili halipaswi kutendwa.

6 Na nilipokuwa hapo, ikaja Sa—Sauti iliyonena nami na kunichukua juu, nami nikaona Maskani haya karibu katika hali yalivyo hivi sasa. Lakini kulikuwako watu wengi sana hadi walijazana ndani kote, Maskanini, katika hali hii, karibu kama ilivyo sasa. Na—nami nilikuwa na furaha, nikisimama nyuma ya mimbara, nikisema, "Mungu, u mwema vipi kunipa Maskani."

7 Kisha, wakati huo, Malaika wa Bwana alinizungumzia, akasema, "Lakini haya si Maskani yako."

Nami nikasema, "Basi, Bwana, Maskani yangu yako wapi?"

8 Basi akanichukua juu katika Roho tena, na kuniweka mahali penye kichaka. Na chini huko kichakani kulikuwa na mistari ya miti yenye urefu ulio sawa tu, urefu wa kama futi ishirini, au thelathini. Nayo ilionekana kama miti ya matunda, nayo ilikuwa katika ndoo kubwa mno za kijani kibichi.

9 Ndiposa nikaona kuwa kwenye mkono wangu wa kuume na kwa mkono wangu wa kushoto, kulikuwako ndoo tupu pande zote mbili, nami nikasema, "Na hizi je?"

10 Naye akasema, "Unatakiwa kupanda katika hizo." Kwa hivyo nilivunja tawi toka kwa mkono wa kulia na kuliweka kwenye ndoo ya upande wa kulia, na tawi toka kwa mkono wa kushoto na kuliweka kwenye ndoo ya upande wa kushoto. Ikakua yote upesi hata angani.

11 Ndipo Yeye akasema, "Nyosha mikono yako na kusanya matunda yake." Na katika mkono mmoja kukaangukia tofaa kubwa manjano, zuri na lililoiva. Na katika mkono mwingine kukaangukia tunda kama zambarau kubwa la manjano, zuri na lililoiva. Naye kasema, "Kula tunda lililomo, maana ni la kupendeza." Nami nilikula toka kwa mmoja kisha kwa mwingine, tamu sana. Mwajua ono hilo limeandikwa katika mojawapo ya vitabu, nadhani, *Hadithi ya Maisha*, au *Nabii Azuru Afrika*.

12 Mara tu nikainua mikono yangu, na nilikuwa nikishangilia utukufu kwa Mungu. Kwa ghafla, ile Nguzo ya Moto ikashuka juu ya miti hiyo, na ngurumo na umeme ukaangaza, na upepo ukavuma kwa nguvu sana na matawi yakaanza kupepea toka kwa miti. Nami nilitazama kule chini, hapa lilisimama umbo la Maskani haya, jinsi yalivyo sasa. Na mwishoni mbapo mimbara ingekuwa, kulikuwako miti mitatu, na hiyo miti mitatu ilichukua umbo la misalaba mitatu. Nami nikaona kuwa matunda kama zambarau na matofaa yalikusanyika katika kichala kuuzunguka msalaba wa katikati. Nami nikakimbia mbio, nikilia kwa sauti yangu yote, na nikaangukia msalaba huu, au karibu na huo msalaba, na kuukumbatia. Kisha upepo ukaanza kutikisa, na lile—lile tunda toka msalabani, likaniangukia. Na nilikuwa na furaha sana, nikifurahi tu. Kisha akasema, "Kula tunda lake, maana ni la kupendeza."

13 Ndiposa huu mzunguko wa Moto ukaitana ukisema, "Mavuno yameiva, na watenda kazi ni wachache." Naye akasema, "Basi ukipata fahamu tena, au ukitoka kwa hili, soma II Timotheo 4. II Timotheo 4." Basi nikapata fahamu. Nami nilisimama hapo nikipangusa uso wangu kwa mikono yangu. Kwa ghafla, pembeni mwa kile chumba, huku jua linang'aa sana, ndipo huenda nilikuwa katika ono kwa saa moja au zaidi, kisha ikasema, "II Timotheo 4." Basi nikaitwaa upesi Biblia yangu, na kusoma II Timotheo 4.

14 Sasa, ningependa kusoma hayo basi. Na ajabu kama ionekanavyo, niliposoma hii II Timotheo 4, mahali nilipokomea, na ambapo mara nyingi nimehubiri juu yake hapa Maskanini, ajabu ni kwamba kila mara ningekomea hapo. Sasa katika II Timotheo 4, vile vifungu vitano vya kwanza. Ambavyo, tano ni hesabu ya "neema." Nasoma haya.

> *Nakuagiza . . . mbele za Mungu na mbele za Kristo Yesu, atakayewahukumu walio hai na waliokufa, kwa kufunuliwa Kwake na kwa ufalme Wake,*
>
> *Lihubiri Neno, uwe tayari wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho.*
>
> *Maana utakufa wakati watakapokataa mafundisho yenye uzima, ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia . . . watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti;*
>
> *Nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo.*
>
> *Bali wewe, uwe na kiasi katika mambo yote, vumilia*
>
> *mabaya, fanya kazi ya mhubiri wa Injili, timiliza huduma yako.*

15 Je, uliwahi kutambua, na sikuitambua hadi huu mwezi uliopita wa Mei, sikusoma Maandiko hayo zaidi ya hapo? Hayo tu ndiyo niliyoyasoma tu kwa sababu hayo yalionekana kuwa yata—yatosha, kwa sababu yaliniambia nihubiri Neno na kuvumilia mabaya, na kuwa mvumilivu, maana wakati ungekuja ambapo watayakataa Mafundisho yenye uzima, lakini kwa kuzifuata tamaa zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti, na wangegeuka kuacha Kweli na kuziendea hadithi za uongo. Lakini, sasa, Yeye hakuwahi kusema mimi nilikuwa muhubiri wa Injili. Yeye alisema, "Fanya kazi ya mhubiri wa Injili." Paulo akimwambia Timotheo, mwaona. Je, mliona jinsi isemavyo? Yeye hakusema, "Sasa umeitwa kuwa mhubiri wa Injili." Alisema, "Fanya kazi ya mhubiri wa Injili." Mwaona? Sasa, tunaona, hapo basi. Naam, kama ningesema kwa moyo wangu wote na kwa kufahamu kwangu kwote, hayo yametimizwa vilivyo. Vivyo hivyo hasa. Na hiyo ni miaka thelathini iliyopita.

16 Na kama nijuavyo mimi, kila ono Yeye alilonipa limetimia ila lile lililosema ningebadili huduma yangu, hata ambapo nitawaombea watu katika mahali padogo kama kijumba kidogo chini ya hema, au ukumbi mkubwa au kitu fulani. Ilionekana kwangu, kama hema. Je, mnakumbuka hilo, miaka miwili au mitatu iliyopita? Karibu lote lilitimilika. Ilinibidi kwenda kule Mexico, na jinsi kungenyesha usiku huo na kile kingetendeka chini kule. Naye alinieleza huduma yangu ya ule mvuto wa kwanza. Mnakumbuka kuhusu kule kuvuliwa kwa vile vijisamaki, au kuvikosa? Wa pili ulikuwa samaki wadogo. Lakini Yeye aliniambia, "Katika ule mvuto wa tatu, usikosee. Mwaona? Na usiwaambie watu." Mimi kila mara nimejaribu kueleza kile ninachojaribu kufanya. Yeye aliniambia nisiwaambie watu kile unachotenda. Nitende tu kile Yeye ananiambiacho nitende na kukiacha pekee. Mwaona?

17 Lakini mimi ni mtu wa aina hiyo, sina siri, kwa hivyo mimi hueleza tu yote ninayojua. Basi, huo, huo ni ukoo tu, nadhani. Lakini huo, najaribu . . . Nawapenda watu, nami nawataka watu waokolewe sana hata hujaribu kuwaeleza kila kitu ninachojua, ila tu iwe ni jambo fulani aliloniambia nisiseme, naam, ili wasije wakalikosa. Mnaona? Nawataka walione kwa makini sana hata kusiwe na kosa lote ndani humo.

18 Sasa, hilo lilitimilika vivyo hivyo. Sasa kumbuka, agizo lilikuwa, ikiwa tutajifunza tu hilo kwa muda mchache, "Nakuagiza mbele za Mungu, na mbele za Bwana Yesu Kristo, atakayewahukumu walio hai na waliokufa, kwa kufunuliwa Kwake na kwa Ufalme Wake." Mnaona? "Hukumu . . . nakuagiza mbele za Mungu, na mbele za Kristo, kuwa—kuwa ulihubiri Neno." Na kwa hivyo anisaidie, hadi usiku huu, kwa kadiri ninavyofahamu, sijahubiri cho chote ila Neno, mwaona, na kudumu Kwalo. Imekuwa shida sana, nami nimepitia katika

mateso mengi na majaribu mengi, ilinibidi kujitenga na marafiki wangu wapendwa kwa ajili ya fungu hilo la maneno, "Lihubiri Neno." Nami ni—nimefanya hivyo.

19 Mwakumbuka katika ono langu, au nikuite uhamisho mdogo, majuzi, ambapo nilitwaliwa na kuwaona watu hao na kujitazama mwenyewe na mamilioni hao wote pale. Kisha nikasema, "Nataka kumwona Yesu."

Naye akasma, "Yeye yuko juu zaidi."

20 Vema, mnaona, watu wanapokufa, wao—wao hawamwendei Mungu mara moja. Sasa, ninyi, nina hakika utafahamu hilo. Labda yanibidi kueleza vema niwezavyo. Mna haraka basi? Na tuchukue wakati wetu basi na—na—na kujaribu kuifanya dhahiri niwezavyo.

21 Sasa, tujapo tunakumbuka kuwa twaishi hapa katika viwango vitatu. Na sijui kama ninaweza kuvitaja au la. Kimoja ni nuru, na kingine ni vitu. Tommy, unakumbuka kile cha tatu ni nini, ahaa? Atomi, wakati. Vema. Naam, nuru, vitu na wakati. Na zile hisi zetu tano huwasiliana na hivyo viwango. Kuona kwetu huwasiliana na nuru, kugusa kwetu huwasiliana na vitu, na kadhalika.

22 Sasa, lakini tuna uwasiliano wa sayansi, kile *kiwango cha nne*, kama ilivyo. Kwa sababu zikipitia papa hapa jengoni sasa zaja picha, sauti za redio, picha za televisheni, ambazo hisi zetu haziwasiliani nazo, walakini wana bo—bomba au kioo kinachoyachukua hayo mawimbi ya hewa nyepesi sana na kuyadhihirisha. Kwa hivyo, mwaona, mumu humu jengoni mna matendo ya watu yanayotendeka sasa hewani, sauti zinazosikika sasa. Ziko hapa. Tunajua hivyo. Ni za kweli hasa. Na jambo likupasalo kufanya, wao—wao wanazinasa kwa . . . Sielewi maarifa ya—ya vitu hivyo ambavyo sayansi imevumbua, lakini twajua kuwa inatuthibitishia sisi kuwa kuna kiwango cha nne.

23 Sasa, kile *kiwango cha tano* ni ambapo mwenye dhambi, asiyeamini hufa na kwenda. Kile kiwango cha tano ni, vema, kiwango cha kuogofya. Sasa mtu huyu . . .

Na Mkristo anapokufa, huingia katika *kiwango cha sita*.

Kisha Mungu yuko katika *kiwango cha saba*.

24 Sasa basi, mwaona, Mkristo anapokufa, yeye huenda chini ya madhabahu ya Mungu, moja kwa moja hadi katika Uwepo wa Mungu, chini ya madhabahu. Na yeye anastarehe.

25 Kuifafanua. Mtu awapo na jinamizi, yeye hawi amelala kabisa, wala hawi macho. Yeye yuko katikati ya usingizi na kuwa macho, na hiyo ndiyo humfanya yeye kutetemeka na kupiga mayowe ya kuogofya, kwa sababu yeye hayuko usingizini, wala si macho. Na ukichukua hilo, laonyesha mtu aendako akifa kabla hajaongoka. Yeye tayari amemaliza wakati wake, ameisha

kufa duniani, naye hawezi kwenda katika Uwepo wa Mungu, kwa sababu yeye hafai kwenda kule bila ile Damu. Naye amenaswa, na hawezi kurudi duniani kwa sababu wakati wake hapa duniani umekwisha, naye amenaswa katikati, na yuko katika jinamizi. Mwaona? Yeye hawezi kwenda katika Uwepo wa Mungu, kupumzika. Na hawezi kurudi, kuja duniani, kwa sababu wakati wake umekwisha. Yeye yuko katika jinamizi, na ataishi hivyo hadi siku ya hukumu. Jambo la kuogofya kuwa ndani yake, mwaona.

26 Na sasa katika ono hili, naamini nilitwaliwa hata kwenye hicho *kiwango cha sita*, nikitazama chini hapa na ningeona nyuma. Mnaona, kuona si hasa kwa macho ya duniani. Lakini kuona ni jambo kuu kuliko...Kuona waliko nako huko, kuwasiliana kwao huko kuko zaidi ya kuwasiliana kwo kwote ambako hisi zetu za kawaida zaweza kuwasiliana.

27 Hapo wakati mfupi uliopita nilikuwa nikieleza hayo. Nilikuwa nikitazama picha za televisheni ambapo walimtelemsha mtu, nadhani maili mbili au maili moja chini ya bahari, nao walikuwa na miale ya nuru iliyopenyeza. Wao walikuwa wakionyesha wanyama wa baharini. Na hapo wakaja samaki, hao viumbe walioonekana wa kuogofya. Kule, ni usiku wa manane, kulikuwa kweusi kama wino. Nao walikuwa na madini kama nta yanayong'aa gizani juu ya mapua yao na hawakuwa na macho. Sasa, ilibidi walishwe, kwa hivyo ilionekana kama kupata chakula chao, waliongozwa na hisi nyingine; si kuona, kwa sababu hawakuwa na macho, hawangeyatumia huko chini. Lakini wao waliongozwa na hisi nyingine kusudi wapate kufikia vyakula vyao. Nami nilidhani, "Kama ningalimwongoza maskini samaki huyo kwa kuona kwangu, ningempa chakula chake zaidi mno na kumwongoza mahali—mahali, kuona kwangu ku mara nyingi zaidi ya dira yake imwongozayo." Mwaona? Nami nilidhani, "Laiti ningelimwongoza tu!"

28 Ndipo likanijia, "Ikiwa ningejisalimisha tu mwenyewe kwa Mungu, ni zaidi jinsi gani kuona kwa busara za Mungu, ambaye angetuongoza sisi zaidi sana ya vile vitu tuvionavyo, kwa sababu ile imani ambayo Yeye hutupa sisi ni bayana ya vitu visivyoonekana, kwa macho yetu." Ndipo ikiwa samaki huyo mdogo hangeweza kamwe kuja juu ya maji kama samaki wengine, kwa sababu ametiwa pumzi. Mlete juu, yeye atapasuka. Vivyo hivyo hatuwezi kwenda juu zaidi na tusipasuke. Tumewekwa pumzi kwa kutuwezesha kuwa—kuwa mahali tunapoishi.

29 Lakini sasa ikiwa maskini samaki huyo angewahi kuja juu hapa na awe mimi, je, yeye angependa tena kuwa maskini samaki huyo chini humo kwenye giza la usiku wa manane? Yeye hangetaka kuwa tena samaki, kwa sababu yeye yu kitu fulani kikuu zaidi ya samaki, yeye ni mtu; hisi zake ni kuu

zaidi, kufahamu kwake ni kukuu, maarifa yake ni ya hali ya juu sana. Ndipo jumlisha hayo na milioni kumi, ndipo unapata vile ilivyo uondokapo huku na kuingia katika Uwepo wa Mungu huko, ambamo mwanadamu yu mbali zaidi kuliko tulivyo hapa. Hungependa kuwa mwanadamu kama huyu tena, chini hapa katika nyumba ya magonjwa na uharibifu. Imekuwa hivyo moyoni mwangu, kwamba nimejaribu hii miaka thelathini kuhubiri Injili kote duniani, kuwaambia watu kuwa kuna Mbinguni za—za kupata na kuna kuzimu ya kuepa, na kuna Mungu akupendaye, na ngu—nguvu za ukombozi zilizowekwa tayari kukuinua wakati wo wote uwapo tayari kuzipokea.

30 Kama mtu anayezama, kamba ikining'nia hapo, yeye adhani, "Vema, kamba ile, ningejitoa mwenyewe, lakini sistahili kupata kamba." Kamba hiyo iliwekwa hapo kwa kusudi lile, ile wewe ujivute mwenyewe toka huko. Hiyo ndiyo sababu Yesu Kristo alikufa, kusudi awaokoa wenye dhambi. Naye alining'iniza kamba ile ya Uzima wa Milele ambayo usiku uu huu itapitia juu ya kichwa cha kila mwenye dhambi humu, na ishara ya kukaribisha iking'inia juu yake, "Njoo, utoke kwake." Iki—ikiwa wewe—ukiwa unataka kufanya hivyo, matayarisho yamefanywa.

31 Sasa, nilipoona mahali hapo na hali hiyo ambayo watu hao walikuwamo, na jinsi zaidi ya kitu cho chote ambacho ulimwengu huu ungewahi kuwazia, palikuwa penye utukufu. Hakungeweza kuwa na dhambi huko, wala kifo, wala hakuna cho chote kingeingia mahali hapo. Na hakukuwa na tofauti, kati ya mwanamume na mwanamke, ila tu ile—ile hali ya kiume au ya kike ilikuwa imewatoka na hakungekuwa tena na uzinzi wala cho chote kile. Lakini yeye alikuwa angali mwanamke kwa maumbile, na mwanamume kwa maumbile, na daima watakuwa hivyo. Kwa sababu Mungu alipo-. . .

32 Sasa hili laweza kuwa zuri, wengine wenu walio watoto wa shule ya upili mnaopata kufunzwa upuzi huu kuhusu mageuzi yenye kuendelea. Naam, naamini katika mageuzi yenye kuendelea, lakini si eti mwanadamu aligeuka toka—toka kwa jamii ya viumbe wa hali ya chini. Nadharia yao huwapinga wenyewe wanapojaribu kuchanganya mbegu zo zote, haitaweza kujizaa yenyewe tena. Kwa hivyo, mwaona i—inawapinga wenyewe.

33 Sasa, naamini kuwa Mungu alipoanza kuijaza dunia, labda kitu cha kwanza alichoumba kilikuwa ni yavuyavu, na toka kwa huyo mpaka kwa chura, na kuendelea juu. Lakini, mwaona, kila mara ilizidi kukaribia zaidi mfano wa mwanadamu, na mwanadamu alikuwa mfano wa Mungu. Na hiyo ndiyo sababu nyasi huwa na mageuzi yanayoedelea, labda nyasi, ndiposa toka kwa nyasi maua, na toka kwa maua vichaka, toka kwa vichaka miti. Kwa nini? Ni mfano wa ule Mti wa Uzima ukisimama upande wa pili. Na kila kitu upande huu kilicho cha kawaida

ni kivuli cha ya Kimbinguni au yale ya Milele kule ng'ambo. Kwa hivyo, mradi tu kuna Mkristo aliyezaliwa mara ya pili duniani na tuna mwili hapa ulivyo hivi, ni onyesho la ule unaongoja kule ng'ambo ambako hakuna kifo wala huzuni. Na hilo ndilo lifanyalo mioyo yetu iwe na njaa kwa ajili ya jambo kama hilo. Mnaona, kuna kitu fulani ndani yetu kinachoita. Sisi hu-. . .Kuna kitu fulani kitwambiacho sisi kuwa upo. Naamini kwa miaka hii yote. . .Naomba msamaha mbele za Mungu na za watu, kwa kuwa mjinga na kwa kuwa. . .kufanya makosa mengi. Lakini kwa miaka hii mingi nimeshajaliwa kuwaona watu milioni nyingi wakiingia katika Ufalme wa Mungu, na ninamshukuru Bwana kwa kuniruhusu kuwaongoza wao huko. Nami naamini watakuwa huko siku hiyo.

34 Sasa, ono lile lilitimia. Na jinsi nilivyoendelea na kukomea, bila kujua, kwa kile kifungu cha 5. Hayo tu ndiyo niliyowahi kuyasoma. Lakini kuna mengine zaidi katika sura hiyo, vifungu vingi zaidi. Sasa, labda wewe, katika chumba chako hotelini au nyumbani usiku huu, mara tu tutakapowarahusu kuondoka, soma yaliyobaki yote, kwa sababu nina Maandiko kadha yaliyoandikwa hapa ninayotaka kuyataja, na muhtasari wa maneno ninayotaka kuyataja. Nami nataka mkayasome muendapo nyumbani. Nitayanukuu, yatakuwa kwa kanda. Mkitaka kuandika baadhi yake, naam, itakuwa sawa.

35 Sasa, je, mwaamini kuwa wanaume na wanawake, nami najua mnafanya hivyo, wanaongozwa na Roho wa Mungu kutenda mambo? Mwaona? Na Yesu alikuwa kielelezo chetu. Ukiangalia, nataka kufungua, fungueni pamoja nami, katika Injili ya Luka Injili ya Luka Mtakatifu, sura ya 4, kwa dakika moja hivi. Nami nataka kuwaonyesheni kitu fulani cha ajabu. Ili tu tusipate kutaja mafungu haya mengi, ili tu mpate kusoma pamoja nami hapa, hili tu, kwa muda mchache. Luka Mtakatifu, sura ya 4 na kifungu cha 14, tuanze. Sasa chunguza kwa makini hapa ukitaka kuona kitu fulani kikitendeka, hili likiambatanishwa. Sasa tazama.

> *Yesu akarudi kwa nguvu za Roho, akaenda Galilaya,. . .Yeye akarudi katika nguvu za Roho, akaenda Galilaya, habari zake zikaenda katika nchi zote za kandokando.*
>
> *Naye alikuwa akifundisha katika masinagogi yao, akitukuzwa na watu wote.*
>
> *Akaenda Nazareti, hapo alipolelewa, na siku ya sabato akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi yake, akasimama ili asome.*
>
> *Akapewa chuo cha nabii Isaya, akakifungua chuo, akatafuta mahali palipoandikwa, palipoandikwa,*
>
> *Roho wa Bwana yu juu yangu, kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma*

kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, na vipofu kupata kuona tena, kuwaacha huru waliosetwa,

Na kutangaza mwaka wa BWANA uliokubaliwa.

Akakifunga chuo, . . .

36 Sasa, ukitaka, ukitaka marejeo yake, ninayo hapa, kwa muda mchache, ikiwa nitaweza kuyapata kwenye maandishi yaliyoko kandoni mwa kurasa hapa. Ukitazama, hayo pia utayapata katika Marko na mahali mbalimbali lakini, katika Isaya 61:1 na 2. Sasa, si ni ajabu kuwa Yeye alikomea tu papo hapo, na kifungu kifuatacho . . . Hicho ndicho kilichotumika katika kuja Kwake kwa kwanza. Na kile kifungu kinachofuata, kinahusu Kuja Kwake kwa pili, hukumuni. Yeye alikoma hapo na kukifunga kitabu kile. Ikiwa ye yote wenu anasoma Biblia nakala ya Scofield, utapata maelezo yaliyoandikwa chini ya karatasi kukihusu. Mwaona? Tazameni maelezo yenu yaliyoandikwa chini ya karatasi ya alama "2," maelezo, mwaona, na maelezo yaliyoandikwa chini ya karatasi, na utaona hapo ulinganifu na ule—ule ujumbe uliotajwa katika Isaya 61:1 na 2. Mm . . . wakati wa . . . ambapo Maandiko hapa, akiuhubiri, Yesu alihitajika ahubiri ule mwaka uliokubalika wa Bwana; na kile kifungu kinachofuata kinaeleza Kuja Kwake na ile hukumu. Mwaona? Na mwaona jinsi Yeye alikomea papo hapo.

37 Na jinsi sikutambua hilo, na jinsi kila mara nilikomea kwa hiki kifungu cha 5, "Maana utakuja wakati watakapoyakataa Mafundisho yenye uzima, ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti, nao watajiepusha wasisikie yaliyo Kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo. Bali wewe, fanya kazi ya mhubiri wa Injili, timiliza huduma yako." Mwaona? Na kwa msaada na neema ya Mungu nimejaribu kufanya hivyo. Nami nataka marafiki wangu, hapa na huko nje katika nchi ambamo kanda zitakwenda, kusudi la kuchukua msimamo ambao ninao kwa Neno, ni kusudi lili hili. "Lihubiri Neno." Hiyo ndiyo sababu singekubaliana na kanuni za imani zo zote, madhehebu yo yote, kwa sababu nimeagizwa na Mungu kukaa na Neno. Sasa ikiwa mtu mwingine ye yote ataka kufanya kingine cho chote, hayo ni juu yao.

38 Na ukitazama, katika ono ambalo nimekuwa nalo kuhusu huduma yangu, ilikuwa sijawahi kupita miti hiyo. Sijawageuza watu kutoka dinini mwao wanifuate. Sijasema, "Ninyi nyote wa utatu mwe wa umoja" au "ninyi nyote wa umoja mwe wa utatu." Nimepanda katika vyombo vyao wenyewe. Bila shaka. Nilienda kwa wa utatu, nilikwenda kwa wa umoja, nilikwenda kwa kila mtu, na kukaa katikati na sikujiunga na ye yote wao; bali nilikaa katikati, nikiwa ndugu, vivyo hivyo kama ono vile lilivyoniambia nifanye. Na nimekula tunda toka pande zote, wokovu kwa pande zote mbili.

39 Na sasa, je, mlitambua, kuna watu wengi wa utatu wanaoketi hapa, kuna watu wengi wa umoja, na kuna watu wengi mbalimbali. Lakini ungekuwa mdogo vipi kugombania hayo, kwa sababu ikiwa sehemu moja ya ono hilo ilikuwa kweli, sehemu ile nyingine ni kweli, pia. Matunda yote mawili yalipatikana msalabani. Mwaona, yote mawili yalikuwa msalabani yamekusanyika pamoja, na yote mawili tanda kama zambarau na pera, tunda kama zambarau na tofaa yaliniangukia kama mvua huko. Yote mawili. Yote yalipatikana msalabani, kwa sababu hao wote walimwamini Mungu nao wamejazwa na Roho Mtakatifu, na wana kazi za Kikristo na ishara zikiwafuata.

40 Sasa, madhehebu hayatahusikana nayo kwa vyo vyote. Itakuwa waliozaliwa mara ya pili ndio watakaohusika nayo kwa vyo vyote vile. Itakuwa ni ujuzi wako na Mungu utakaohusikana nayo. Sasa, twaona mengi sana ya hayo. Nina Maandiko kadha hapa ambayo ningependa kuyataja. Labda nitayataja hivi punde.

41 Lakini sasa nataka kuwachukua toka kifungu cha 5, na kuendelea mpaka kifungu cha 18. Na sasa kwa kuokoa wakati, si—sitayasoma. Lakini sasa Paulo, akianzia hapa katika Timotheo tena, ukitazama jinsi yeye anavyoanza kunena, inahuzunisha. Sasa ukitazama baada ya kifungu cha 5.

> *Kwa maana, mimi sasa namiminwa, na wakati wa. . .kufariki kwangu umefika.* Anakaribia kuondoka machoni pa watu. (Anaanza, waona, “Nime. . .vema, tazama, wa-. . .”) Niko tayari*, na kufariki kwangu kumefika.*
>
> *Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, Imani nimeilinda,*
>
> *Baada ya hayo nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana, mhukumu mwenye haki, atanipa siku ile; wala si mimi tu, bali. . .na watu wote pia waliopenda kufunuliwa kwake.*

42 Halafu anaendelea kueleza “Fanya yote, fanya vitu hivi vyote.” Nini? Amletee lile joho. Sasa tunaanza mara moja, naye anasema:

> . . .*Dema aliniacha,*. . .

43 Hapana shaka kulikuwa na wakati katika huduma yake alipokuwa muinjilisti kijana, nabii kijana, kila mtu alimpenda. Lakini sasa mkiangalia chini hapa, ilisema:

> . . .*Watu wote waliniacha*. . .(Kwa nini? Neno).

44 Wakati Yesu, yule Nabii kijana wa Galilaya, Yeye alifikia wakati alipoachwa. Watu wote wanaodumu kwa Neno la Mungu hufikia mahali ambapo wao huachwa na ulimwengu na ulimwengu wa kidini. Yesu aliwalisha elfu tano, siku

moja, nao wakachukua vikapu vilivyojaa vya—vya mabaki ya mikate mitano na samaki wawili. Na siku iliyofuata, naamini ilikuwa hivyo, Yeye akaanza kuja na Neno, nao wote wakaanza kuondoka Kwake. Basi alitazama hapa na pale kwa wanafunzi, na kusema, "Je! ninyi nanyi pia mwataka kuondoka, pia?" Hata wale wahudumu Wake sabini aliowaweka walimwacha. Naye akasema, "Je! ninyi mwataka kuondoka, pia?"

45 Ndiposa Petro akanena maneno hayo yasiyosahaulika, kwa kusema, "Bwana tungeenda wapi? Wewe ndiwe pekee uliye na Uzima wa Milele."

46 Tazama. Lakini wakati huja ambapo wakati wa kuachwa pekee unakuja, na ya—yapasa uje. Lazima uje. Na sasa nina manabii kadha wa kadha na wengineyo ndani humu wa kuwarejea, kuwathibitishieni ninyi kuwa wakati huo huja. Na umenifikia mimi. Hakuna haja ya kuufutilia mbali, u hapa na lazima uutwae. Hawakuufutilia mbali, wao walisimama na kuutwaa, na sio kuionea haya Injili.

47 Mwamwona Paul, "Nimevipiga vita vilivyo vizuri. Mwendo nimeumaliza. Imani nimeilinda." Lo, jamani! Chini hapa ilisema, "Nimepigana na wanyama. Nami—niliokolewa kinywani mwa simba." Na mambo aliyopitia, Mungu alikuwa mwema kwake. Lakini wakati ulikuwa umefika ambapo yeye angekufa.

48 Sasa, hebu na sisi tustaajabu, mbona mtu, mhudumu, msaidizi kama Dema alivyokuwa kwa Paulo, athubutu kumwacha Paulo?

49 Mwamjua Ndugu Baxter, wengi wenu mwamkumbuka. Yeye alikuwa kila mara akisoma kuhusu Dema. Alisema, "Ndugu Branham, wajua nitakachotenda nifikapo Mbinguni, jambo la kwanza nitakalotenda?"

Nami nilisema, "Lipi?"

50 Yeye alisema, "Nitaenda moja kwa moja na kutafuta alipo Dema, nitampiga kwa nguvu niwezavyo." Na kasema "Yeye atageuka na kusema, 'Baxter mbona ukatenda hilo?'" Yeye alisema, "Mbona ulimwacha maskini mpendwa Paulo wakati kila mtu alipomwacha?" Siyaungi hayo mkono, siamini watapigana huko juu, lakini niliwaza tu kuhusu Ndugu Baxter akisema hayo kwa sababu alimsikitikia sana Paulo.

51 Vema, Paulo alikuwa amefanya nini? Alikuwa amehubiri kwa uaminifu tu jinsi alivyoweza, na Roho Mtakatifu alikuwa juu yake. Na alipoandika hapo kuhusu wale wahudumu wanawake na mengineyo, nakisia kulikuwa na mlipuko. Akasema, "Na wanawake wawe kinya makanisani, siwaruhusu kunena," huku yeye yumo gerezani wakati uo huo.

52 Je, ungewazia yale maaskofu wengine walisema? "Aa! Mtu huyo gerezani huko, ana shughuli gani kutuandikia hapa kwetu?

Waona? Naye ana Timotheo, mlevi wa divai. Na kwa hivyo yeye yuko juu hapo sasa; naye anamnywesha Timotheo divai, huku naye yuko gerezani, anaandika, akitwambia kile Roho Mtakatifu apaswa kutwambia tutende."

53 Lakini yeye alisema haya, "Nini? Neno la Mungu lilitoka kwenu? Kama kutoka kwenu pekee. Mtu ye yote akijiona kuwa ni wa rohoni au nabii, na akubali kuwa yale ninayoyaandika ni Maagizo ya Bwana." Mwaona?

54 Mnaona, wakati huja, marafiki. Nami nawatakeni watu katika nchi ambamo kanda zitakwenda, kukumbuka kwamba wakati wa kutengana unapaswa kuja. Lazima uje. Sijui niko umbali gani toka wakati wa mwisho, wakati wa kufa kwangu. Sijui. Hayo ni juu ya Mungu. Sijui kesho ikoje, wala ni nani . . . Sijui ina nini, lakini najua ni nani anayoishikilia. Kwa hivyo hapo ndipo imani yangu imejengwa, juu ya hayo.

55 Sasa, nadhani Dema hakumwacha na kwelekea kwenye vilabu vya usiku. Siwazii kuwa Dema alifanya hivyo, kwa sababu Dema alikuwa mtu aliyejazwa na Roho. Yeye alikuwa msaidizi mkuu. Kama ungewahi kuchunguza historia ya Dema, yeye alikuwa mhubiri mashuhuri, mtu aliyestaarabika, muungwana sana, mwenye elimu. Yeye alikuwa mtu mwerevu. Lakini mbona yeye angemwacha Paulo? Jambo ndilo hilo. Nini kilimfanya afanye hivyo, kumwacha Paulo? Siamini kuwa yeye alitaka kwenda katika vilabu vya usiku au po pote. Lakini naamini ilikuwa ni Mungu akimtenga Paulo. Sasa nawaza Dema . . .

56 Hebu na tuchukue baadhi ya mawazo ya Dema. Kama nilivyokuwa nimeketi kandoni mwa kilima, nikishangaa juzi juzi, karibu mapambazuko, nami nilikuwa nikiwazia, "Mbona Dema alitaka kumwacha mtu huyo? Mbona yeye angemwacha huyo maskini mhubiri mpendwa aliyemleta kwa Bwana, mtu yule aliyeanzisha ufufuo kati ya Mataifa, nabii halisi?" Hakuna hata mmoja angesema kingine ila tu yeye alikuwa nabii. Yeye alikuwa zaidi ya nabii, yeye alikuwa mtume, na mtume mkuu na mwenye nguvu kwa Mataifa. Na Dema angeshirikiana na Paulo, walikuwa na ushirika na Paulo, na akaona Roho wa Mungu akitenda kazi juu ya huyo. Basi mbona yeye angeachana na mtu kama huyo, aliyekuwa amethibitishwa kuwa alikuwa mtumishi wa Kristo? Je, uliona Paulo hapa, "Akiupenda ulimwengu huu wa sasa." Sasa, sidhani Dema alianguka. Sidhani yeye alifanya hivyo. Lakini nafikiri yeye alipata wazo baya kuhusu Paulo.

57 Naam, Dema alitoka kwa jamii tajiri na alikuwa na mali nyingi, na pesa wakati mwingine humaanisha dini kwa watu. Kama wasemavyo huko California, "Ikiwa huna motokaa tatu za Cadillacs, wewe si wa kiroho." Kwa hivyo yamaanisha, ikiwa haujafanikiwa, ikiwa hamna kanisa nzuri sana mjini, watu hawataenda. Iko karibu hivyo hapa. Pugh. Kwenu—yampasa

mwe na kanisa nzuri sana nchini, au wao watasema, “Wewe, aa, wakusudia kusema ulijiunga na kundi ndogo kama hilo?”

58 Je, wajua Bwana wetu hakuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake? Je, wajua Yeye alikuwa na joho moja tu? Waona? Naye alikuwa nalo. Yeye alikuwa namna ya mtu anayesukumwa huku na huko. Naye hakuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake. Lakini wao wangewaza jambo lile lile, na walifanya hivyo, juu Yake.

59 Naam basi, naamini Dema aliona kushindwa, ilivyoonekana, katika huduma ya Paulo. Nadhani kuwa yeye alidhani mzee huyo amekwisha, mbele za Mungu. Sasa, yeye alidhani kuwa wale watu kwa wangeng’oa macho yao wampe Paulo . . .

60 Sasa, Paulo alisema hivyo, yeye alisema, “Mngeweza, bila shaka, kung’oa macho yenu, mnipe mimi.” Kwa kuwa twadhani Paulo alikuwa na macho mabovu, kwa sababu yeye alisema. “Nimeandika kwa herufi kubwa.” Yeye alisema, “herufi kubwa” lakini nina ile—ile kamusi ya Kiyunani, na inasema “kwa herufi kubwa.” Yeye alikuwa Rumi, gerezani kule. Kulikuwa na kasoro fulani, yeye alisema macho yake yalikuwa yakimsubua tangu lile ono la Kimbinguni. Kwa hivyo yeye . . . Watu wale wangeng’oa macho yao, waona. Na Paulo aumia, macho yake yakimsumbua, naye akiumia. Na alimsihi Bwana amponye, mara tatu. Naye akasema, “Makusudi nisipate kujivuna kwa wingi wa Ufunuo, nilipewa mjumbe wa Shetani ili anipige.” Sasa, angekuwa hajambo sana, kisha angempiga tena. Ndipo angepata nafuu, na angempiga tena.

61 Mwaona, Paulo alikuwa na huduma kuu kuliko ya mitume wengine wote ikiwekwa pamoja. Wengine wao wangesema, “Vema, nimetembea na Yesu.” Naam, watu wa barabarani walitembea pamoja naye alipokuwa hapa. Lakini Paulo alimwona katika ile Nguzo ya Moto baada ya kufa Kwake, kuzikwa, akapaa Mbinguni, na akarudi na kumwita Paulo, mwaona, mwaona, njiani akienda Dameski. Naye alikuwa na huduma kuu kuliko Mathayo, Marko, Luka, au wengineo. Yeye aliwapita. Naye alisema, “Ili nisije nikajiinua sasa na kusema, ‘Sasa ninyi watu hamjui lo lote kumhusu,’ nilimwona Bwana baada ya kufufuka Kwake.”

62 Vema, wao husema, “Tulitembea pamoja naye.” Vema, hata pia na watu wengine kote Galilaya na Nazareti na kote nchini mle. Wao walitembea pamoja Naye.

63 Lakini, mwaona, Paulo alikuwa amenena Naye na kumwona katika hali ambayo Yeye aliyokuwamo kabla hajafanyika mwili. Mwaona? Naye akamwagiza Paulo katika hali hiyo, akiwa katika Nuru hiyo. Akamwagiza Paulo. Na—na Paulo alikuwa amemwona. Naye akasema, “Ili nisijivune, nijisikie juu zaidi yenu ndugu, nilipewa mjumbe wa Shetani,” aliyekuwa anampiga. Naye alisema, “Nilimsihi Bwana mara tatu

aniondolee hiyo. Naye alisema, 'Sauli, au Paulo, Neema Yangu yakutosha.'" Ndipo Paulo akasema, "Nitajisifu kwa udhaifu wangu, kwa sababu ninapokuwa mnyonge ndipo nina nguvu. Mnaona, nitajisifu kwa hiyo!"

64 Naam, ulitambua basi, mtu aliyekuwa na huduma iliyo kuu zaidi ya wengine wote waliowahi kutumika, Paulo, na huduma kuu zaidi ya zote, na ambaye alikuwa amemwona Yesu katika Nguzo ya Moto, na kumwagiza atende aliyoyatenda, na alithibitishwa na Mungu, yule yule, Nguvu zile zile, na ishara na maajabu zaidi ya swali lo lote; naye alikuwa maskini sana hata alikuwa na joho moja tu, akilihubiria kundi la watu ambao wangeng'oa macho yao, wengine wao mamilionia. Hata hivyo, Paulo alikuwa na joho moja. Yeye alisema, "Lete joho hilo, kunakuwa baridi huku." Alikuwa katika nchi ya milima. Alikuwa na joho moja pekee.

65 Kwa Dema, mtu aliyekuwa mashuhuri, wa hali ya juu, mstaarabu, mwenye elimu, na mtu tajiri mwenye mavazi mengi ya kubadilisha, "Mtu huyo, alikuwa na kasoro fulani. Akiwa na marafiki wengi sana ambao wangeling'oa macho yao wampe yeye, na hali yeye alikuwa maskini kupindukia hata ana joho moja. Mna kasoro fulani katika Paulo."

66 Lo, mwajua roho ile haiondoki duniani, wangali wanayo vivyo hivyo. Pesa si Mungu. Kuna Mungu mmoja pekee. Mwaona? Lakini watu hudhani kwa sababu una huduma kubwa yakupasa uwe na yote haya na yale, na vitu *hivi* vikuu na shule kubwa na mkubwa fulani. Mungu hashughuliki na vitu hivyo. Angalau, hayo yamekuwa maoni yangu. Mungu humshughulikia mtu binafsi. Yeye hakutuita sisi kutenda mambo kama hayo.

67 Lakini Paulo, akiwa na joho moja, na anamwambia Timotheo hapa amletee kwa sababu ilikuwa inakuwa baridi kule. Kwani, mtu aliyekuwa na huduma aliyehubiria makumi ya maelfu ambao Paulo aliwahubiria, na huduma ambayo ingetenda kila aina ya miujiza, na kumwona Yesu katika Nguzo ya Moto, na kumwagiza, hata hivyo alikuwa na joho moja tu. Dema alisema, "Mtu kama huyo," akamuacha.

68 Sasa yeye alipokuwa juu hapa akihubiri kuelekea Troa, twaona kuwa kulikuwa na mtu huko aliyekuwa mfua shaba. Naye alikuwa mlaghai. Naye alichukia Ukristo. Naye alitenda kila kitu kwa Paulo ambacho angemtendea, akamfanya atupwe gerezani. Na kila. . .hata Paulo alimwonya Timotheo kuhusu jambo lile lile, "Jihadhari na mtu huyo." Na hapa kuna Dema! Ee Mungu, hebu na watu wayasikie! Hapa alisimama Dema akisimama na mtu aliyempofusha mtu fulani, kwa kubishana naye. Sasa, ninyi wahubiri wa Church of Christ, vaeni majoho yenu sasa. Nilikuwa na mmoja wao wakati mmoja aliyesema, "Nipofushe! Nipofushe! Una Roho Mtakatifu, nipofushe."

Nikasema, "Wewe tayari u kipofu" Mwaona?

69 Sasa, mbona Paulo hakumpofusha yule mfua shaba? Roho yule yule aliyeko juu ya watu wanaowaza hayo, ni yule yule aliyekuwa katika Dema. Mtu ambaye angempofusha mtu mwingine, kwa kubishana naye, kisha ageuke na amwachilie mfua shaba aharibu huduma yake mjini. Hamna shaka Dema alisema, "Yeye, yeye amekwisha, amepoteza karama zake zote. Yeye—Yeye amepoteza kipawa chake cha kupofusha watu."

70 Je, huoni jinsi roho huyo angali anaishi, akasema, "Umekwisha, ndugu"? Jamani! Ina—inapitia tu juu ya vichwa vya watu. Hawaipati, hayo tu. Mwaona? Hawawezi kuona. Mwaona? Hawaelewi.

71 Sasa Dema...hakumpofusha mtu huyo kwa sababu yeye alitaka. Yesu hakusema, "Sifanyi neno lolote Baba asiponionyesha Mimi kwanza"? Sikuwaambia ninyi miaka mingi iliyopita, mama yangu akilala, akifa, na angesema, "Bill, itakuwaje kwangu?" Singesema lo lote ila Mungu aseme hivyo kwanza. Na hivyo ndivyo ilivyotendeka. Mwanadamu hawezi, mwanadamu kwanza ni mshinde. Yeye ni mtumishi tu ambaye Mungu humtumia, na Mungu hutenda mapenzi Yake Mwenyewe. Lakini uonapo hawa watu wanaojingamba mengi ambao kila mara wana *hiki* na *kile* na *kinginecho*, heri usiwakaribie. Waona? Yesu Mwenyewe hakutenda hivyo. Yeye alisema, "Nafanya kazi tu kama Baba afanyavyo. Yeye hunionyesha la kutenda na ndipo naenda kulifanya. Siwezi kufanya kingine...cho chote ila hicho."

72 Na hapa Dema aliona Paulo, mtu aliyekuwa na huduma kama hiyo, na hali alikuwa maskini kupindukia hata alikuwa tu na joho moja, na alimtaka Timotheo amletee. Joho moja! Lakini, Paulo alionyesha mfano kama Kristo alivyokuwa. Yeye alikuwa na joho moja. Basi mbona utajiri na pesa nyingi na vinginevyo huthaminiwa sana na watu siku hizi? Tazama sasa. Alikuwa na nguvu sana hadi mtu ye yote aliyekuwa kinyume cha yale yeye alihubiri alimgeukia na kusema. "Utakuwa kipofu kwa muda." Na mtu huyo akawa kipofu.

73 Na hapa kulikuwa na mfua shaba, aliyemtendea mara kumi zaidi ya yale mtu huyo aliyotenda, hata hivyo hakumtendea na cho chote. Lazima Dema alidhani, "Vema, mwaona, mzee huyo amekwisha sasa. Yeye amepoteza huduma yake." La, la, yeye hakuwa amepoteza huduma yake, hata kidogo. Mungu hafanyi mambo kama hayo. Mungu si mpaji wa Kihindi. Naam. Tazama sasa.

74 Paulo alikuwa mtu wa hali ya Eliya. Nabii Eliya alikwenda mlimani kwa agizo la Mungu, na akaagiza moto ushuke toka Mbinguni, na ukashuka. Naye akaagiza maji, na yakaja. Na kisha akaamru kwa ujumbe wa Mungu na kuua makuhani mia nne, akavikata vichwa vyao na akavifiringisha mlimani, halafu akakimbia kwa tisho la—la mwanamke, maskini

mwanamke mmoja mnafiki, au, alikuwa kafiri. Yezebeli, maskini mwanamke huyo aliyekuwa chanzo cha hayo yote, yeye ndiye aliyeyasababisha. Ilionekana kama kwamba yeye angempata mwanamke huyo kwanza. Lakini Mungu ana njia za kutenda mambo, na watumishi Wake waweza tu kutenda vilivyo ikiwa watatenda kulingana na mapenzi ya Mungu.

75 Hamwoni, marafiki, yawapasa mwenende kulingana na njia za Mungu za kuenenda. Ni mara ngapi nimeketi na ndugu kuwashauri, na jinsi ningependa kuwaendea na kusalimiana nao kwa mikono na kusema, "Ndugu zanguni, si hoja, hebu na tuendela kuwa ndugu." Nitawezaje kufanya hivyo na kutimiza agizo langu, "Lihubiri Neno"? Sitaki kufanya hivyo.

76 Nimesimama kati ya wahudumu, kasema, "Ndugu Branham, shangazi yangu yuko hapa. Najua kuwa wewe u nabii uliyetumwa toka kwa Mungu. Nenda huko ukamrudishie kuona kwake." Laiti ningaliweza, ningelifanya hivyo. Siwezi kulifanya hadi Yeye aniambie nilifanye. Mwaona? Hakuna angaliweza kufanya hivyo. Eliya hangelifanya hivyo, hakuna mwingine angelifanya hivyo.

77 Sasa twaona ya kwamba Paulo . . . Dema akihubiri na Paulo, alikuwa amemwona Paulo akimwona mtu aliyelemaa akilala pale, na kusema, "Naona una imani ya kuponywa. Simama kwa miguu yako! Yesu Kristo akuponya." Alikuwa amemwona akiponya wagonjwa, na hata hivyo alimwacha rafiki yake Theofilo akiwa mgonjwa.

78 "Paulo amepoteza huduma yake." Hivyo ndivyo ilimlazimu Dema kudhani. "Mbona yeye, ikiwa yeye alikuwa na karama ya uponyaji, mbona yeye hakwenda kule na kumponya huyo mwenziwe aliyesimama pamoja naye kwa'NimememwachaYeye alisema, 'Nimemwacha huko hawezi. Na sina joho, pia nakutaka wewe uniletee joho hilo. Na ujihadhari na huyo mfua shaba, yeye aliuharibu ule mkutano mjini. Ilinipasa niondoke mjini humo. Yeye alinitupa gerezani.'" Nadhani Dema alisema, "Huyu amekuwa mhubiri wa aina gani?" Mwaona?

79 Na, ndugu, kuna roho wengi wa Dema duniani siku hizi. Hawajui ni nini. Mwaona? Hakuna haja kujaribu kueleza hayo kwao, kwa sababu hawatayafahamu kwa vyo vyote. Mwaona? Mwaona? Mtumishi wa Kristo hufuata zile Nyayo.

80 Mmoja wa mashemasi hapa, sijui kama yeye ako hapa usiku huu au la, ni Tony Zabel. Yeye kila mara huwa humu. Basi alinijia na kusema hapa si muda mrefu uliopita kabla yeye kupata—akaja hapa; akasema—yeye akasema, "Nilikuwa na ndoto, ndoto ya ajabu." Akasema "Ni—niliota nikijaribu kutafuta njia ya kwenda juu Mbinguni." Akasema, "Nilimwona mtu akija amevalia joho jeusi na alikuwa aki—aki—akisoma kitabu." Kisha akasema, "Ni—nilimwendea mtu huyu, na kumwuliza, 'Ni njia gani iendayo 'Mwulize?' Basi akasema, 'Mwulize mtu aliye

mbele yangu." Na huyo alikuwa mch—mchungaji wa kanisa alilohudhuria.

81 Yeye aliendelea mbele kidogo na akamkuta mtu mwingine, aliyekuwa amevalia joho jeusi na akiimba nyimbo, akiendelea. Huyo alikuwa mchungaji mwingine. Wachungaji hao wote wawili ni marafiki wangu. Naye alisema . . . Watu wazuri. Basi akauliza, "'Nitapitia njia ipi nifike kwenye kilele kile cha mlima hapa?' Akasema, 'Tazama hapa.' Kasema, 'Waona, yule mtu mdogo aliyesimama juu kule kileleni?' Nikasema, 'Naam.'" Kasema, "Hapo kulisimama mtu aliyevalia surupwenye na mojawapo ya kofia zile ndogo za wachunga ng'ombe."

82 Mtu fulani alisema chini huko Kentucky, alisema, akinena kunihusu mimi, huko, alisema, "Mtu huyo anaonekana kama kitu cho chote ila mhubiri." Huenda aonekana kama mkulima au ye yote yule, lakini—lakini, mwajua, si sura.

83 Na kusema kuwa ilikuwa mimi niliyesimama juu huko. Basi aka—akakwea juu mpaka akanifikia, akasema nilimshika mkononi na kumwongoza juu hadi nikafikia kilele cha mlima. Na kulikuwa na jangwa la kupitia. Nami nilisema, "Tony, yanipasa nikuache hapa na lazima upitie baadhi ya hii wewe mwenyewe."

Yeye akasema, "Ndugu Branham, nifanyeje toka hapa na kuendelea?"

84 Kasema nilisema, "Njoo hapa, Tony, tazama chini kule. Waona zile alama za nyayo tupu zenye Damu?" Nilisema, "Hizo ndizo nimefuata wakati wote. Kaa tu Kwake." Hilo ndilo jambo pekee najua kumwelekezea mtu, si kanuni ya imani wala mwamsho wa aina fulani, lakini kwa hizo Nyayo zenye damu ziongozazo Bibliani, ile Damu ya Yesu Kristo.

85 Sasa, jinsi mtu huyo angejisikia, mtu aliyekuwa na marafiki wengi mamilionia, na joho moja. Mtu aliyekuwa . . . aliyekuwa na nguvu ya kumpofusha mtu, na huku amwachilie mtu mwingine amfukuze mjini. Hakumtendea jambo lo lote, aliinuka na kutoka nje. Aliwaombea wagonjwa kisha akamwacha rafiki yake mgonjwa. Kisha Dema akamwacha. Na wengine wote walimwacha. Wao wote walimwacha. Paulo alisema, "Watu wote wameniacha." Kila mmoja wao alimwacha.

86 Nasema haya. Mtu adumupo mwaminifu kwa Neno, si kwa mkutano mmoja tu, bali katika kila mkutano, mtu adumupo mwaminifu kwa Neno, wakati utakuja ambapo watamwacha. Hakika. Wao walifanya hivyo. Wao walimfanyia hivyo Bwana wetu. Watamwacha yeye anaposimama katika Kweli. "Watu wote wameniacha." Na sasa wadhani Dema na baadhi ya watu hao waliwaza nini hali sote twajua, tunaojua Maandiko, kuwa Luka alikuwa daktari, na Paulo, ko kote alikoenda, aliandamana na daktari huyu? Na akihubiri uponyaji wa Kiungu, huku akimwacha rafiki yake mgonjwa. Maskini sana, yeye alikuwa

na joho moja. Na kuachilia mtu amfukuze mjini, hali yeye angempofusha mtu. Mnaona, wao walidhani yeye amekwisha. Lakini yeye hakuwa amekwisha! Yeye alikuwa hasa katika zile Nyayo za damu. Yeye alikuwa akizifuata tu. Nadhani mnafahamu. Yeye alisema, "Watu wote wameniacha."

87 Dema, akipenda ulimwengu huu wa sasa, kupendwa na watu. "Salaam, Daktari Dema. Najua ulipata cheti chako cha Ph.D!"

88 Ee, hakika, wao hupenda hilo. Yesu alisema, "Jinsi mnavyopenda kusimama katika masinagogi, na kuitwa 'Rabi,' na kadhalika." Kasema, "Mnapokea tu hukumu zaidi." Mwaona?

89 Sasa, twajua walipoona huyu daktari akimfuata au akiwa pamoja naye, na Paulo alimchukua Luka, akasema yeye alisema—alisema hapa, "Luka yuko—Luka ndiye pekee ambaye hakuniacha." Na Luka ni—ni mzuri kwake. Lakini Luka anamfaa sana. Yeye anahitaji Luka katika huduma yake. Na daktari huyu akimfuatilia mtu kokote alikoenda, huku anahubiri uponyaji wa Kiungu. Mtu ambaye alihubiri uponyaji wa Kiungu na angewaponya vilema na kuwafufua wafu, na mambo mengineyo, na kuona maono makuu, na kunena mambo ambayo yangetendeka, na amwache mfanya kazi mwenziwe akiwa mgonjwa. Na angepata dolla milioni na ajenge majengo yanayogharimu makumi ya maelfu ya dolla, na shule kuu na kadhalika na hakuwa na joho ila moja la kuvalia mgongoni mwake.

90 Dema alisema, "Sitashirikiana na mtu kama huyo. Yeye ni—ni mtu wa hali ya chini. Nitaambatana na ndugu wa kidhehebu. Nitakwenda huko ambako nitakuwa mtu mashuhuri." Ikiwa ilikuwa kitu kama hicho, ningependa kutembea, na hata baada ya Baxter kumaliza, mwaona, kwa kumwacha maskini mtu huyo katika hali hiyo. Ilimpasa Yeye kumsaidia. Paulo alikuwa ndiye aliyemuongoza kwa Kristo. Lakini, mwaona, ni pasipo kumjua Roho, kujua mapenzi ya Mungu ndiposa kutenda mapenzi ya Mungu. Mwaona? Sasa, lakini hapo yeye alimwacha katika hali hiyo. Akamwacha! Watu wote walimwacha.

91 Jinsi niwazavyo kuhusu hilo! Jinsi mtumishi atakayedumu mwaminifu kwa Neno, hakuna budi, kumbuka tu, watu watamwacha. Sasa, twataka kugusia hilo tu kwa dakika chache, na sitawakawisha sana sasa, kwa sababu nawatakemi ninyi hapa asubuhi. Kila mara mtumishi wa Mungu amapodumu mwaminifu kwa Neno, wote humwacha. Na hu-. . . Sasa, chukua po pote unapotaka, wakati wo wote katika Biblia au katika historia, kuwa mtu alipodumu mtiifu kwa Neno, haidhuru alipendwa vipi na watu, alipodumu kwa Neno, wakati ulifika ambapo ulimwengu wa kidini ulimwacha na kumkatilia mbali. Sasa, hebu soma tu uchukuapo Biblia toka Mwanzo mpaka

Kitabu cha Ufunuo, na uichukue toka Kabla ya Baraza la Nikea ukafikie wale Wazee wa Nikea, na kila mtu, kila mtakatifu, kila nabii, kila mtumishi wa kweli wa Mungu aliyelitii Neno, alikataliwa na makanisa kisha akafukuzwa. Na Paulo alikuwa mmoja wao.

92 Na ikiwa kungekuwa na mmoja leo, lingekuwa jambo lile lile. Ni kweli hasa. Huna budi ufikie mahali hapo. Hauna budi uje. Wao hudhani kuwa mtu ambaye angekuwa na huduma kama hiyo, yampasa kuweka ulimwengu chini ya kidole chake. Yampasa, lakini hawatakuwa chini ya kidole chake. Mwaona? Na mtu kama huyo hangeiweka huduma, ulimwenguni chini ya kidole chake; yeye angeuweka chini ya kidole cha Bwana wake, kwa sababu yeye hayuko hapa kujiwakilisha mwenyewe, yeye anamwakilisha Bwana wake.

93 Mwajua, mwanadamu hujaribu kutafuta heshima mmoja kwa mwingine, nao huheshimiana, na kutokumheshimu Mungu kwa kufanya hivyo. Mwaona? Tunajaribu kujifanyia watu wakubwa kati yetu, na hali sisi si watu wakubwa na wadogo, sisisote tu watu wadogo. Kunaye mmoja tu aliye mkubwa kati yetu, na huyo ni Bwana wetu. Ona? Nasi hufanya madhebu yetu makubwa zaidi kuliko Mungu, "kanisa kuu takatifu la *huyu, yule* au *mwingine*, maaskofu wakuu watakatifu," na kadhalika. Hakuna kitu kama hicho. Hiyo ni heshima ya mwanadamu. Kunaye Mmoja pekee aliye mtakatifu, na huyo ni Mungu. Na Roho Mtakatifu, ambaye ni Mungu, yuko kati yetu. Si sisi tulio wataktifu, ni yule Roho Mtakatifu aliye ndani yetu. Si . . . Tuonapo mambo yakitendeka, si sisi tunaotenda, ni Roho Mtakatifu. Yesu alisema, "Si Mimi nifanyaye kazi, ni Baba Yangu. Yeye aishi ndani Yangu, na Yeye ndiye afanyaye hizo kazi." Na si yeye ambaye—ambaye anayezitenda. Vema. Lakini twawapata hao watumishi waaminifu kote katika wakati.

94 Sasa hapa kuna kitu ambacho nataka nikieleze kwa muda mfupi. Naam, kila mara ni wakati kama huu ambapo mtu amekaa mwaminifu kwa Neno na watu wote wamemwacha ndipo Mungu aingiapo amtetee mtu huyo na kuivika taji huduma yake. Mwaona? Hiyo ni kweli. Ni faraja jinsi gani! Faraja zetu zimejengwa katika ahadi za Neno la Mungu. Haiduru ulimwengu wasemaje, kile ulimwengu utendacho, hayo siyo matumaini yetu, hayajengwi juu ya yale ulimwengu unatenda.

95 Nafikiri wimbo huo ni mzuri sana. Laiti ningeliuimba. Kila mara nilitaka kuuimba. Mwaona? "Wao wamngojeao Bwana, watapata nguvu mpya; watapanda juu kwa mabawa kama tai; watapiga mbio, wala hawatachoka, wakienda kwa miguu hawatazimia, nifundishe, Bwana, kungojea. Nifundishe Bwana kungoja magotini mwangu." Napenda hayo. "Na kwa wakati Wako ufaao utajibu maombi yangu; unifundishe nisitegemee yale wengine watendayo, lakini kungoja tu kwa maombi jibu litokalo Kwako." Naam. Huyo ndiye mtumishi mwaminifu

angojeaye zamu ya Bwana wake, akijua hili, kuwa Maandiko hayawezi kushindwa, bila kujali kipi kitendekacho. Maandiko hayana budi kudumu kweli. Katika wakati kama huo ndipo Mungu mara nyingi huingia kuwasaidia.

96 Hebu tumtazame Eliya alipoachwa. Kwani? Kwa sababu yeye alikuwa amekaa mwaminifu kwa Neno. Yeye alisema, "Watu wote wameniacha." Na yeye alitengwa na umma, na madhehebu, na hata madhehebu ya kitaifa, au kanisa la taifa la Israeli, makuhani na wengineo walikuwa wamemtupa nje, na yeye hakuwa hata na joho kama Paulo, lakini kipande kidogo cha ngozi ya kondoo, akaketi juu mlimani na kulishwa na ndege. Naam, bwana. Kwani? Kwa ajili ya lile Neno la Mungu, kwa sababu yeye alikuwa mwaminifu kwa BWANA ASEMA HIVI. Naam, hao wote wamekuwa wa kisasa. Mwanamke wa kwanza nchini, Yezebeli, alikuwa na mitindo yote na mengineyo. Na makuhani walikuwa wameikubali na kadhalika, na wahubiri wote na kadhalika, walishirikiana katika hayo. Lakini si Eliya, yeye aliishi mwaminifu kwa hilo Neno. Na kwa jambo kama hilo yeye akaachwa, hadi akalia, "Bwana, mimi pekee yangu nimesalia, nao wanaitafuta roho yangu."

97 Lakini Mungu alimpa faraja kidogo, kasema, "Bado ninao elfu saba chini huko."

98 Mwaona, sidhani Eliya alijiinua kwa ajili ya hilo, kuwa yeye alikuwa ndiye pekee, lakini nadhani aliachwa tu. Kila wakati yeye angeenda kwa kuhani afanye mkutano, wangemfukuza. Yeye alikwenda hapa chini. "Ondoka hapa, ewe mshupavu wa dini! Ondoka, nenda zako! Nenda kafanye *hiki*!" Ilijidhihirisha Elisha alipokuja, yule aliyemfuatia. Vema, walifanyaje? Wao hata. . . Yule mtu kijana alikuwa na upara, nao waliwatuma watoto wao wadogo kuwafanyia mzaha hao wazee "walaghai." Wote wawili walidhaniwa walaghai, kasema, "Mzee upara! Mwenye upara, mbona, hukupaa kwenda juu kama vile Eliya alivyofanya?" Hawakuamini yeye alikwenda juu. A-haa. Mwaona? Wao walidhani tu ni kundi la walaghai. Lakini wao walikuwa waaminifu kwa Neno, pamoja na huduma iliyothibitishwa. Eliya alisimama. Vema.

99 Danieli alichukua msimamo wa kweli. Mwajua ninapopata hilo katika Danieli 12, au ni Danieli 9, naamini. Unapo. . . Danieli alichukua msimamo halisi wa Neno. Nini kilitendeka kwake? Yeye alipokuwa mtu wa pili toka kwa mfalme, lakini yeye alichukua msimamo wa kweli kwa Neno, naye akafukuzwa na kutupwa kwenye tundu la simba. Mtu wa Mungu akisimama mwaminifu kwa Neno!

100 Wale watoto Waebrania walidumu waaminifu kwa Neno, chini ya tangazo la mfalme kuwa "ye yote ambaye hatasujudu sanamu hiyo wakati zeze ipigwapo na baragumu iliapo na kadhalika, ye yote asiyesujudu sanamu hiyo atatupwa

katika tanuru ya moto," nao waliipa ile sanamu kisogo. Kisha wao—wao, bila kujali wanadharauliwa vipi, bila kujali watafukuzwaje toka kwa umma, wao walikuwa waaminifu kwa Neno. Napenda hayo.

101 Yakobo, mwingine. Yeye alikuwa . . . alikuwa amekuwa mbali na nyumbani kwa muda mrefu, naye alikuwa na wito kwenda nyumbani kuwaona watu wake. Naye akashika njia, mwaminifu kwa wito wake, mwaminifu kwa kuongozwa kwake. Yeye alikuwa na mambo mazuri kule, lakini Mungu alianza kumfanya atake kwenda nyumbani. Na akiwa safarini kwenda nyumbani, alitupwa kati ya mahali pawili paliposonga. Mke wake na watoto upande huu, na ndugu yake aliyemchukia, Esau, akija hapa na jeshi kumlaki. Na yeye alisimama hapo karibu na kile kijito, kijito cha Penueli pale, naye akasimama hapo. Na ni hali jinsi gani! Esau, akimchukia, akija na jeshi kumlaki, na huyu hapa mke wake, wake wawili na watoto wote upande huu wa kile kijito, naye alikuwa mahali paliposonga sana. Kwani? Kwa sababu kama yeye angalikaa katika nchi yake mwenyewe ingekuwa sawa. Lakini yeye alikuwa na wito, Neno la Mungu lilimwita arudi katika nchi yake. Haleluya! Mungu ambariki mtu. Yeye alipata badiliko pia. Naam, bwana.

102 Yesu, mwaminifu kwa Neno la Baba, "Nafanya tu yale ambayo Baba husema. Imeandikwa, 'Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo kinywani mwa Mungu!'" Yesu, mwaminifu daima kwa lile Neno, ulifika wakati ambapo Yeye aliwapoteza marafiki zake wote aliokuwa nao. Kila mmoja wao alimwacha akaondoka. Wao wote. Na watu waliomwona walimdhihaki, wakamfedhehi, wakapoteza imani naye. Yawezekanaje mtu ambaye angemsema na mtu mfu kaburini na kumfufua, yawezekanaje mtu ambaye angetabiri mambo kikamilifu na hajawahi kuwa na . . . isikose kutimia, na aketi mahakamani uso Wake ukiwa unatokwa na damu tokana na kung'olewa ndevu, na mate yenye harufu mbaya toka kwa wanajeshi walevi yakitiririka usoni Mwake, wakimzungushia kitambaa kichwani mwake, na kumgonga kichwani kwa kijiti, na kusema, "Tabiri na ukatwambie ni nani aliyekugonga, nasi tutaamini"? Naam, hao wanafunzi waliondoka tu, wakisema, "A-haa."

103 Mnaona, wao husahau upesi yale Mungu aliyofanya! Jinsi Musa alivyosema huko kwenye Bahari ya Shamu, aliposimama hapo na kusema, "Mungu ametenda miujiza kumi isiyosahaulika, je mngali wakosaji sana hata msijue kuwa Yeye yungali Mungu yule yule?" Yeye alishuka akaenda huko na kushinda nchi, yeye—yeye aliweka laana nchini. Alileta vyura, chawa, inzi, kila kitu, na m—mlipuko uliowaua wazaliwa wote wa kwanza, na yule malaika wa mauti alipitia nchini, hata hivyo watu hao hawakutaka kumfuata huko, kwenye Bahari ya Shamu. Ni upesi jinsi gani, mara tu kupendwa

kwako. . .Walipoiona hii mikuki mikubwa iliyong'aa ya watu elfu mia wakija hivyo, au labda, naam, labda watu milioni moja wakija, au mlio wa hayo magari na mavumbi yakipeperuka, wao walikata tamaa na kurejea nyuma. "Basi, Musa, heri tungefia huko." Waona? Na Mungu alisema Yeye aliwaacha wafe jangwani kwa ajili ya kutokuamini. "Musa, huduma yako imekwisha, hivyo tu. Wewe siwe tena." Mwaona, hawafahamu. Hawalipati.

104 Na sasa jambo lile lile lilikuwako wakati Yesu, yule Rabi kijana, au Mwalimu, au Nabii wa Galilaya, alipokuwa akifanya miujiza hiyo yote na mengineyo, "Yeye angesimamaje na kustahimili jambo kama hilo? Yeye angewezaje kumwacha mtu amfunge kwa minyororo, hali Yeye angevunja ule muhuri wa kaburi na kufufua wafu toka Umileleni? Angestahimilije, na huku angesema neno kwa mtoto wa mwanamke mjane aliyekufa na kumfufua apate kuishi; na Lazaro, aliyekufa na akaozea kaburini, kisha akamtoa huko? Yeye angewezaje kusimama, aseme, 'Mimi ndimi Ufufuo, na Uzima. Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi. Naye kila aishiye na kuniamini hatakufa kamwe!' Na asimame na kufungwa na minyororo na kutemewa mate usoni Mwake, na asifungue kinywa Chake"? Wale wanafunzi, "Yeye amepoteza huduma Yake." Naam, hivyo ndivyo iendavyo. Mungu, huu ulimwengu maskini!

105 Hata kanisa Lake, wale kumi na wawili ambao Yeye aliwafurahia na kuwaambia kila kitu, na kuwapenda. . . Walimpa kisogo. Mmoja tu ndiye alisimama pamoja naye, huyo alikuwa yule mtu aitwaye Yohana. Papo hapo kwa saa ambayo kila kitu kilikwisha, na tumaini lote lilikuwa limekwisha, hapo yeye alikuwa amefungwa pingu, na kupelekwa juu hapo na kudhihakiwa na kutemewa mate, na kuelekeza mgongo Wake. . . Bila kujua kuwa hilo lilitimiza Maandiko.

106 Vema, hamjui kuwa mambo yanayoendelea siku hizi yanatimiza Maandiko kabisa? Mbona watu huacha. . .wao husema mambo hayo? Mbona madhehebu haya yanafanya ghasia? Mbona wao hufanya hivyo? Imeandikwa katika Maandko watafanya hivyo. Wao hutembea moja kwa moja hadi kwa hiyo na kuifanya wenyewe, vipofu wala hawajui wanalifanya. Wadhani Yuda alijua alikuwa akitimiza sehemu ya Yuda? Wadhani Farao alijua alikuwa akitimiza sehemu ya hiyo, na Mungu alimwinua kwa kusudi hilo? Mwadhani Esau angetenda mambo aliyoyatenda. Hasha kabisa. Kasema, "Wana macho na hawaoni, masikio na hawasikii." Lakini chunguza Maandiko, yanafunuka. Mwaona? Tuko katika wakati wa mwisho. Haina budi kuwa hivyo.

107 Naam, kanisa Lake lilimwacha. Watu wote na maumbile yalimwacha. Nena kuhusu mtu kuachwa, Paulo hakuachwa kama Yeye alivyoachwa. Hata viumbe alivyoviumba Yeye vilikuwa vinamwacha, mwezi na nyota na jua na kila kitu,

zili zimika. Mwanadamu, Mungu, maumbile na kila kitu kilimwacha, hakuna kilichosimama pale, Yeye alikufa peke yake. Je, Yeye alipoteza huduma Yake? Alikuwa akitimiza huduma Yake, si kuipoteza. Hayo huandamana nayo. Hilo ndilo jambo litendekalo. Hilo huandamana nayo.

108 Sasa, kila kitu kilimwacha. Lakini ilikuwa wakati huu ambapo Mungu alitokea wazi, kwa sababu mtu ye yote ajuaye Neno atakaa na lile Neno, akijua kuwa Neno ni Mungu. Mwaona? Na Neno halina budi kujifunua Lenyewe. Lile Neno lisilokosa kutimia lazima lijifunue Lenyewe. Linapaswa liwe, katika taratibu, kwa sababu Neno ni Mungu. Na ikiwa lilitende kwa wengine kote katika zile nyakati, litafanya vivyo hivyo hivyo sasa, kwa sababu ni Mungu. Usisahau hilo kamwe. Maana Yesu alijua kuwa Yeye akiwa ukamilifu wa Neno, Yeye hakuwa tu nabii, alikuwa Mungu Mwenyewe. Yeye alikuwa Neno. Hiyo ndiyo sababu si mwanadamu tu aliyemwacha, bali hata maumbile yalimwacha. Maumbile yote yalimwacha Yeye, kila kitu, nyota, mwezi, na hakukuweko nuru Yeye alipokufa. Kila kitu kilimwacha, mwaona, kwa sababu Yeye alikuwa Muumba wa vitu vyote. "Alikuwako ulimwenguni; hata ulimwengu uliumbwa na Yeye, na ulimwengu haukumtambua." Mwaona? Yeye alikuwa Muumba wa vitu vyote. Vitu vyote! Sasa, jambo pekee, ambalo sisi—sisi hatuumbi lakini tunajaribu kuongoa, na wale tunaojaribu kuwaongoa ndio wanaotuacha na kuondoka. Mwaona? Wakati unapowadia kwa Neno kujidhihirisha wazi kabisa hapana budi iwe hivyo. Sasa, kumbuka tu, hapo, ndipo Mungu atokeapo wazi.

109 Na katika maisha ya Bwana wetu Yesu, zile kazi kuu alizozifanya katika ule mwaka wa kwanza na miezi sita ya maisha Yake, lo, jinsi Yeye alivyokuwa mtu mkuu! Hakukuwako na cho chote kama Yeye duniani, hakujakuwako tangu wakati huo, na hakutakuwako baadaye. Lakini nini ilitendeka? Yeye alipata dhihaka zaidi ya wengine wote, wakiwekwa pamoja. Alidhihakiwa na maumbile na akadhihakiwa na viumbe, alidhihakiwa na kila kitu, kwa sababu vilikuwa katika hali iliyepotoshwa. Hiyo ndiyo sababu mioyo ya watu ilimdhihaki mtumishi halisi wa Mungu, kwa sababu imepotoshwa. Maumbile yamepotoshwa, hiyo ndiyo sababu.

110 Ikiwa maumbile ni mazuri jinsi yalivyo, hali yamepotoshwa, je, yatakuwaje yakigeuzwa kurudia mapenzi ya Mungu? Ikiwa nchi yaweza kuzaa zabibu zinazohitaji watu wawili kuzibeba mgongoni mwao, itakuwaje, na hiyo ni nchi iliyopotoshwa, itakuwaje ikigeuzwa kumrudia Mungu? Kristo ajapo, jangwa zitachanua kama waridi. Itakuwa badiliko. Na mahali pakavu patabubujika maji, na nchi itatoa maua na kustawi. Lo, huo utakuwa wakati wenyewe, wakati mioyo ya watu itakapoongoka iwe ya watu wacha Mungu, ambao wamekuwa wakikata kauli yao sasa, wataishi mahali pale. Amina.

111 "Katika saa hiyo yenye giza, huku miamba ikipasuka na anga zikiwa giza," kasema mwana mashairi, "Mwokozi wangu alikiinamisha kichwa Chake akafa; ile pazia iliyofunguka ilifunua njia ya kuelekea rahani za Mbinguni na siku isiyo na mwisho." Yeye alipaswa kufanya hivyo ili atutengenezee njia. Naam. Lakini Mungu alifanyaje? Yeye alikuwa mwaminifu kwa Neno, na akaukumbatia msalaba. Lakini, je, ulikuwa mwisho wa huduma Yake? Je, huduma Yake ilikwisha? Mungu aliivisha taji kuu zaidi ambayo ingaliweza kuvishwa. Yeye aliivisha taji asubuhi ya Pasaka, wakati wa kufufuka. Yeye aliitimiza huduma ya Bwana Yesu, akafufuka toka kwa wafu na yu hai hata milele. Yeye hakumalizwa kwa sababu watu wote walimwacha, alitiwa taji! Naam, bwana. Naam, bwana. Yeye alivikwa taji kwa sababu alikuwa, alikuwa ameachwa, naye alilazimika kufanya hivyo alipomfufua katika wafu.

112 Ilikuwa vivyo hivyo kwa Eliya. Tulinena juu yake dakika chache zilizopita. Eliya, huyo maskini nabii mzee aliyechoka akilala hapo jangwani, na alipaswa alishwe kwa kile ndege wangemletea. Na mwili uliokonda na kukunjamana, ulioonekana wa hudhurungi, chupa yake ndogo ya mafuta ikining'inia ubavuni mwake, masharubu yake yote yamekua, na kichwa labda upara na kimechomwa na jua, akienda huku anachechemaa, akiwa na fimbo *hivi*, lakini chini ya ule moyo maskini uliozeeka, Roho wa Mungu alipiga-piga. Mungu alipomwona mtumishi Wake mzee mpendwa anakaribia kufa, kila mtu amemwacha, na kila kitu kinginecho, je, Yeye alimuaibisha? Yeye alimtelemshia gari likamchukua juu mtumishi Wake aliyechoka, "Haikupasi hata kutembea kwenda juu kama Henoko alivyofanya, nitakupeleka tu nyumbani katika gari." Hiyo ni kweli. Yeye alivisha taji huduma yake kwa kumpeleka nyumbani kwa gari. Hilo si baya sana, mwajua. Naam. Naam, haikumpasa kutembea mpaka nyumbani. Yeye alituma tu gari likamchukua kwa sababu alikuwa amechoka. Napenda hilo. Amina. Maskini mtumishi mpendwa, aliyezeeka, na mchovu, Yeye alimchukua akampeleka Nyumbani.

113 Na kwa wakati ule tu Danieli aliposimama ali mwaminifu sana kwa Mungu hata akaingia. . . Wao walisema, "Mtu huyo, mwajua, wakati mmoja yeye alikuwa mtu mkuu hapa katika ufalme huu. Yeye ametabiri mambo mengi mbalimbali. Naye amewaingiza ndani wanajimu, akawafundisha mambo." Na wale Waamedi na Waajemi na yale aliyofanya. Lakini chini ya utawala wa Dario, Danieli ndiye aliyekaa mwaminifu kwa Mungu. Ilikuwa Danieli aliyekaa na Neno la Mungu na hangechanganyikana na cho chote kile. Naye alisema, "Vema, huduma yake imekwisha, kwa sababu niliiona katika gazeti la hapa, yeye atatupwa kwenye tundu la simba katika siku chache zijazo." Atapelekwa katika Gereza kuu la serikali, au kitu cho chote kile, mwaona. "Lakini tutamtupa katika tundu la simba."

Lakini Mungu alifanyaje? Mungu aliitia muhuri huduma yake kwa kuugeuza moyo wa mfalme, hata Dario akatumana kwa kila lugha, watu kote duniani, kuwa kila mtu lazima amche Mungu wa Danieli, kwa sababu Yeye alikuwa Mungu ambaye angeweza kuokoa. Amina.

114 Kwa hivyo, mwaona, ni katika wakati huo ambapo watu humwacha mtu, watumishi wa Mungu wanaokaa waminifu kwa Neno, ndipo Mungu hutia muhuri huduma zao kwa wakati wa kuvishwa taji.

115 Naam, ilikuwa wana Waebrania chini ya utawala wa Nebukadreza, wakati hawangesujudu ile sanamu. Wao walikaa waminifu kwa Mungu kwa sababu Neno la Mungu lilisema, "Msisujudu sanamu yo yote, mkaiabudu." Wao walikaa waaminifu kwa Neno. Na ilikuwa kwenye gazeti la nchi ile, katika taarifa ya habari, kila kitu juu yake, cho chote kilichokuwa katika, siku hizo. Wao walikuwa na njia za kueneza habari. Si katika magazeti ya nchini, sivyo hakika, nasema tu hivyo ili mfahamu. Lakini ilikuwa ndani humo ambako wao walikuwa wanaenda kuwachomwa katika tanuru ya moto iliyokuwa na moto mara saba zaidi. Maana siku nyingi kabla ya hilo, wao walitupa vifaa vyote walivyovipata ili kufanya tanuru ipate moto sana hata ikawa mara saba moto zaidi, ilitiwa moto mara saba zaidi. Vema, ungewateketeza wakifikia yadi mia toka kwake. Lakini wao waliingia moja kwa moja katika tanuru hiyo ya moto, na kutoka toka humo pasipo hata kupatwa na harufu ya moto. Kisha Nebukadneza akasema, "Kila mtu ambaye hatamwabudu Mungu huyu, na watoto wake pamoja naye wauawe, nyumba yake iteketezwe na kufanywa jaa." Hiyo ni kweli. Mwaona? Yeye. . .Wao walikuwa na ufufuo ulioenea duniani kote kwa sababu walidumu waaminifu kwa Neno. Hilo ndilo lililotendeka. Naam, bwana. Kaa mwaminifu kwa Neno, naam, na kila mara litakufaidi kiajabu.

116 Yakobo, tulimtaja kitambo kidogo kilichopita. Niliandika jina lake hapa. Ndiye huyu hapa, mwoga kidogo, lakini alikuwa anakawia. Alikuwa anamwogopa Esau pale. Jamani wee! Naye alijua alikuwa mbali na Mungu. Alikuwa amekuwa mbali na Mungu miaka hii yote, lakini yeye kila mara alijaribu kukaa mwaminifu kwa hilo Neno. Na hapa Mungu alimwita na kumwambia aende nyumbani kwake. Huyu hapa kwenye wajibu wake, na huyo hapo Esau pamoja na jeshi. Ilikuwa wakati huo ambapo yeye aligeuzwa jina toka *Yakobo* "mdanganyifu, mwenye hila," kuwa Yakobo . . . "mtawala mbele za Mungu," alipondoka asubuhi iliyofuata, huku huduma yake ikiwa imevishwa taji. Akaondoka akaenda kumlaki Esau, na hakuhitaji msaada toka kwake. Amina. Mwaminifu kwa Neno. Hivyo ndivyo Mungu afanyavyo mambo, sivyo? Yeye—Yeye hufanya mambo kwa njia Yake. Sawa.

117 Wengi wa ndugu zangu, wanapendwa na watu sana siku hizi miongoni mwa ndugu zao wa kimadhehebu. Utamke tu jina moja, wee, ni tu kama moto, popote, hiyo ni kweli, taja jina fulani la mtu huyu. Na hata hivyo, Bwana aliponena nami huko mtoni siku hiyo, ilitangulia ufufuo huo kote ulimwenguni, toka hapo kukaja kila mmoja wa hao wahubiri wakuu.

118 Wao walirudi nyuma huko pamoja na ndugu zao, mwaona, yale madhehebu walimotoka. Wanakuja nje hapa na kufanya mkutano huu, wakichanganyikana na madhehebu, na kurudi mumo humo tena. Wanapendelewa sana, majina makubwa redioni, magazetini, na kila kitu. Kila mtu anena mema juu yao.

119 Lakini watu wote wameniacha kwa sababu nilichukua Neno la kweli, na kusimama na Neno lile. Nimedumu papa hapa kwa yale Yeye aliyoniambia mimi, nikahubiri Neno, si filosofia ya kidhehebu. "Lihubiri Neno," hilo ndilo lililokuwa agizo langu, "kaa na Neno." Basi ndugu zanguni, mnaosikiliza kanda hii, nilikuwa mtu mashuhuri nilipokuja kati yenu, nikiponya tu wagonjwa, nikinena juu ya maono na kuwaonyesha mambo. Lakini nilipoanza kuwaambia ile Kweli kuhusu Neno, mbona mlinipa kisogo? Je, mnatambua ni kutimiza tu yale Maandiko yalisema? Naam, inafanya hivyo. Sasa ni vigumu kwangu kuingia mahali popote.

120 Barua huja wakati wote. Moja ilikuwa juzi, ikasema, "Ndugu Branham, nilikuwa na imani kubwa sana nawe, lakini nilikusikia ukisema dhehebu fulani nililomo lilikuwa likianguka." kasema, "Sasa sina tena na imani kwako hata kidogo, tangu sasa na kuendelea." Kasema, "Kulikuwako na ndugu wa dhehebu langu wapatao ishirini na watano walioketi katika mojawapo wa mikutano yako," Kasema, "tulisimama tu—tulisimama na kuondoka uliposema hayo."

121 Vema, watu wote wameniacha, lakini kuna kitu kimoja, Yeye alisimama pamoja nami! . . . ? . . . Mimi si, sikuliasi lile ono la Mbinguni lililotokea huko mtoni. Nimelitii. Yeye amekuwa mwaminifu kwangu. Namtumainia Yeye siku moja, sijui lini, kuivisha taji huduma yangu. Nitakaa mwaminifu niwezavyo. Sijui itakuwaje, sijui itakuwa lini. Nami . . . Lakini Yeye awapo tayari, mimi niko. Sasa tazama hapa. Natumaini Yeye ataivisha taji huduma yangu hivi kwa kuniruhusu mimi nichukue nguzo za Neno, na kumvika Bibia-rusi Wake katika vazi la Neno, na kwa ajili ya haki Yake. Natumaini Yeye atanivika taji na kuniruhusu nisimame hapo siku hiyo, na kusema, "Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu."

122 Kuna vilima vingi sana vya kupanda kwenda juu, ile juhudi, wakati mwingine huwa vigumu; lakini Yule aonyeshaye njia, ajua tu kile kilicho bora sana. Yeye ajua kilicho bora sana. "Taabu za njiani zitaonekana kama si kitu, tufikapo mwisho wa njia." Hebu nasi tutafute hizo nyayo zenye damu. Kumbukeni

tu, marafiki, "Changarawe zimejaa nyayo za yule Mgeni kwenye ufuo wa bahari ya Galilaya; na sauti hiyo iliyonyamazisha yale mawimbi, haitasikika tena katika Uyahudi. Lakini njia ya huyo Mgalilaya mpweke, nitaifuata leo kwa furaha; na taabu njiani zitaonekana kama si kitu, nifikapo mwisho wa njia."

123 Katika sehemu hii ya kwanza ya Maandiko niliyosoma, Yeye aliponipa, nilikuwa kijana, mvulana tu, nikisimama kule nje, huku mabega yamenyoka, kifua mbele, mwenye vunga la nywele za matao, nyeusi. Na sasa nasimama mabega yameinama, mwenye upara, mwenye mvi, mzee wa umri wa miaka hamsini na mitatu. Lakini Yeye anazidi kuwa mtamu zaidi siku zinavyopita. Nami sijaacha kuwatangazieni ninyi Injili yote ya Yesu Kristo. Na shauko ya moyo wangu ni kukutana na Kanisa ambalo Yeye amelifia, limevikwa haki ya Damu Yake Mwenyewe, limevikwa Neno Lake na haki ya Neno Lake, maana Neno halishindwi kamwe. Hivyo basi, najua ikiwa nitasimama na Neno na kuwa wa kweli kwa Neno, na kama Neno atakaa ndani yangu nami ndani Yake, siku hiyo nitafurahia kwamba niliishi mwaminifu.

124 Sijui ya usoni yanachoshikilia, lakini mwaona tulipo, sivyo? Mwaona sababu kila mtu anasema, hata baadhi ya wenzi wangu, kasema, "Mbona, Ndugu Branham umekwisha." Mwaona? Naam. "Amekwisha kabisa." Mwaona? "A-haa, hatusikii mengi zaidi yakifanywa." Mwaona? vema, sisi . . . Wao hawafahamu, hivyo tu, hawafahamu, mwaona.

125 Nadhani jambo kuu sana ambalo Paulo alitaka, yeye aliposema, "Sasa wakati wangu umekwisha," hamu kuu sana ya moyo wa Paulo ilikuwa kuwa mfia imani. Hiyo ilikuwa hamu ya mioyo yao wote siku hizo. Ikiwa wao . . . Je, mmewahi kusoma *Kitabu cha Fox cha Wafia Imani*, na pia kusoma *Lile Baraza la Nikea?* Heshima kuu ambayo ingekuwa, wakati watu mbali mbali (na Polikapu na wengineo) walitembea hadi tunduni mwa simba, wao walishangilia. Waliingia ndani humo wakijua kuwa watakuwa wafia imani. Walipochomwa moto hali wamefungiwa mtini, walipiga mayowe kwa furaha kwa ajili ya heshima ya kuwa wafia imani. Paulo alipotembea kuelekea mahali pa kukatia kichwa, ili wakakate kichwa chake, wakimpeleka mle gerezani, mahali padogo pachafu chini hapo, shimo ukutani, walipomweka yeye. Nilienda mle, nikapatazama, ghuba ndogo zee nyuma huko ambamo waliutumbukiza mwili wake. Na sasa wanataka kumfanya mtakatifu au kitu fulani kile. Kundi lile lile la watu! Pale akatembea mle chini. Yeye alisema, "U wapi, Ewe mauti, uchungu wako? Ku wapi, Ewe mauti, kushinda kwako? Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye ushindi kwa Bwana Yesu Kristo. Nimevipigana vita vilivyo vizuri, mwendo. Nimeumaliza. Imani nimeilinda. Nimewekewa taji, wala si mimi tu, bali na watu wote wanaopenda kufunuliwa Kwake."

126 Sasa tumefikia kile kifungu cha 6, mpaka cha 18. Sijui itasomekaje kwangu, lakini nawanukuulieni inavyosomeka

kwa wengine. Na nitaendelea kukaa mwaminifu kwa Neno mpaka Yeye amalize. Hapo ndipo huduma ilipo siku hizi. Sijakwisha. Natumaini nimeingizwa katika yule Mfalme. Naam. Na tuinamishe vichwa vyetu tunapoomba . . . 9

127 Kunayo kamba ndogo ambayo imefika chini toka kwenye kile Kiti cha Enzi usiku huu, inaitwa Kamba ya Kuokolea. Huku nikiomba, natumaini inapitia pole pole kwa kila mtu asiyeongoka ndani humu. Mbona usiifikie na kuishika, rafiki mwenye dhambi? Wasema, "Ndugu Branham, ulisema unazeeka, nami nadhani hiyo ndiyo sababu una-. . . " La, ndugu, dada. Nilipokuwa tu mvulana mdogo, niliamini Hili. Nimetoa uhai wangu kwa ajili ya Hilo. Na kuna sikitiko moja pekee nililo nalo, sina ila tu uhai moja wa kutoa. Kama ningekuwa na uhai elfu kumi ningependa kuutoa wote kwa ajili ya Hilo, Kwake.

128 Je, mbona usishike hiyo Kamba ya Kuokolea ipitapo karibu nawe usiku huu, mahali ulipo? Unasema, "Ndugu Branham, sistahili kuishika." Najua hustahili mwanangu. Lakini nenda kafanya jambo fulani upate kustahili, kisha uniambie uliyotenda, mimi pia nataka kufanya hivyo. Hakuna jambo uwezalo kufanya ili ustahili. Ulizaliwa usiyestahili. Kuna kitu kimoja tu uwezacho kufanya, hebu tu shika ile njia uliyotengenezewa. Wewe unazama, usizamie humo. Mungu amekutupia Kamba ya Kuokolea, hebu—hebu na tuifikie na tuishike usiku huu.

129 Baba yetu aliye Mbinguni, nakumbuka papa hapa kwenye meza ii hii, mahali papa hapa niliponena asubuhi hiyo, ambapo niliweka wakf kanisa juu ya ardhi hii hapa. Na hilo jiwe la pembeni liko pale, bado lina ile karatasi ya Biblia niliyoandika hayo. Nilisema, "Bwana Yesu, kwa neema Yako nitakaa mwaminifu kwa Neno." Na sasa naona limezaa kile hasa limefanya katika nyakati zingine. Na mimi hapa katika Maskani haya usiku huu, baada ya kusafiri dunia nzima, na kurudi tena, na hilo jiwe dogo la pembeni bado liko mle na karatasi ile iko ndani yake. Nichunguze, Bwana. Nime—nimefanya makosa mengi. Nime—nimefanya mabaya. Bwana. Mara nyingi nimekukosea Wewe, kama nilivyoshuhudia muda mfupi uliopita kuhusu kosa. Mungu, mi—mimi, mara tu nitendapo na—na—nataka msamaha. Moyoni mwangu nakupenda. Nami na—najua ulinionyesha hivi majuzi kuhusu mahali pale tunapoenda. Na sasa sijui lini utakapomaliza nami, Bwana. Ni—niko hapa usiku huu, kwa neema Yako, na si—sijui lini utakapomaliza, lakini najua hili halina budi kufikia hili. Lakini ifikapo wakati huo, si—sitaki kuwa mwoga. Nataka kusimama kama wengine wao walivyosimama. Lakini, Mungu, ikiwa—ikiwa—ikiwa yanipasa kutia muhuri ushuhuda wangu kwa uhai wangu, au cho chote kile, Bwana, ivishe taji basi. Si kunivisha taji mimi; ivishe taji huduma ambayo nimehubiri, Bwana, ni Neno Lako. Nami najua Neno hilo linaweza kabisa kunifufua mimi tena katika ule

ufufuo. Na silionei haya Neno ambalo nimehubiri, kwa sababu ni uweza wa Mungu uletao wokovu kwa wale wote waaminio.

130 Nakushukuru kwa ajili ya kanisa hili ndogo ambalo lingali linasimama hata wa leo. Nilipochukua msimamo huo kwa ajili ya Neno, nao manabii walitabiri na kusema, "Katika miezi sita litageuzwa gereji." Miaka thelathini imepita, na liko sasa na moto kuliko lilivyokuwa kwa miaka mingi, "juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu." Twakushukuru kwa ajili ya mchungaji wetu. Twakushukuru kwa ajili ya mashemasi, wadhamini. Sisi sote tuna sehemu ndogo ya kutimiza, Bwana, nasi twataka kuitimiza kwa uaminifu, twataka kuifanya vizuri.

131 Huenda kunao wengine ndani humu wanaotaka kuungana nasi usiku huu, Bwana. Na jinsi wajiungavyo, ni kushikilia tu hii Kamba ya kuokolea na kuendelea kuvuta, kuifungia mkononi mwao, na kuifungia moyoni mwao na kusema, "Sasa, Bwana, univute, niinue juu," nao watajitokeza na kung'aa kama dhahabu. Tujalie, Bwana. Tunautazamia wakati huo.

132 Tunaamini kuwa mwisho u karibu. Twaona ya kwamba kama vile tumekuwa tukifundisha hapa, ule Wakati wa Kanisa la Laodikia sasa unaendelea, twaona hakuwezi kutendeka kitu kingine ila kule Kuja kwa Bwana. Na, Bwana, si huko kungekuwa kutimilika kukuu kwa Neno, kumwona Utimilifu Mwenyewe akija? Ningependa niwe nimesimama hapa na kusema, "Ndiye yule pale, yule pale Mwana-Kondoo." Kama alivyosema Yohana. "Tazama, Mwana-Kondoo ambaye tumemngoja, ndiye huyu." Bwana atakuja upesi kwa hekalu Lake, awachukue watu Wake katika kunyakuliwa.

133 Tufanye tayari, Baba. Isafishe mioyo yetu katika Damu Yako. Tufanye wasafi na weupe, ili Neno Lako likae ndani yetu. Nasi tukumbuke kuwa yatupasa kutenda kulingana na Neno, lishikilie na nguvu na kuleta matokeo. Mpe kila mwenye dhambi toba. Bariki kila mmoja aliye ndani humu. Watakatifu, wale, baadhi ya hawa mashujaa wapendwa wa kale, Bwana, ambao wamekuwa wakipigana kwenye mstari kwa miaka mingi, wamedhihakiwa, wamenenewa na kufanyiwa mzaha. Wao bado wangali wakiendelea kwa sababu wao wana Uzima. Wao wanajua yule wanayemwamini, na wameshawishika Yeye aweza kuyahifadhi yale waliyomkabidhi Yeye. Twakushukuru kwa ajili ya hayo. Twaomba kuwa utawaponya wagonjwa walio kati yetu. Ondoa dhambi zetu zote pamoja na magonjwa. Na, Baba Mungu, jipatie Mwenyewe utukufu.

134 Nina marafiki wengi wapendwa, Bwana. Ni—ninawapenda, nami najua watu wengine wamefanya vivyo hivyo kote katika nyakati. Marafiki wa thamani marafiki wawapendwao, vijana kwa wazee, nasi twawapenda kwa mioyo yetu yote. Sasa tufanye waaminifu, Bwana, waminifu tu kwa Neno, kusudi tukutane nao katika nchi bora siku moja ambako hakutakuwa kamwe

na huzuni wala masikitiko. Twatazamia kule Kuja kwa Bwana, upesi. Twaamini kuwa Yeye atakuja.

135 Sasa bariki asiyeamini hapa usiku huu, Bwana, na yeye awe mwamini na akukubali Wewe kama Mwokozi wake usiku wa leo.

136 Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, ikiwa kungekuwako mtu fulani hali vichwa vyetu vemeinamishwa angesema, "Ndugu Branham, ndani kabisa moyoni mwangu, ni—ninataka nifikie mwisho wangu, nikipigana vita vilivyo vizuri. Nataka kuwa Mkristo. Nitainua mkono wangu." Mungu akubariki wewe, na Mungu akubariki. Hilo ni jema. Mungu akubariki wewe, wewe. "Nataka nifikie kikomo changu, nikiwa na vita vilivyo vizuri nyuma yangu. Ninamkubali Kristo sasa hivi. Namtaka Yeye awe Msaidizi wangu." Vema, Bwana akubariki. Mungu akubariki, bibi uliye kule nyuma. Naam. Yeye—Yeye anakujua. Nimejifunza kutosha juu Yake katika miaka hii yote, karibu miaka thelathini na miwili sasa nyuma ya mimbara, nimejifunza kutosha kumhusu Yesu sasa kujua kuwa Yeye ajua kila hatua uchukuayo. Yeye huona ndege. Nywele za kichwa chako zimehesabiwa. Waona, Yeye ajua hayo yote. Wewe inua tu mkono wako, na likusudie, hilo tu ndilo likupasalo kutenda. Na maji yako tayari.

137 Kumbuka unafanyaje? Unatubu, amini Injili, ndiposa ubatizwe. Kwa—kwa nini? Katika Jina la Yesu Kristo, upate ondoleo la dhambi zako. Huo ndio ushuhuda wako, ya kwamba zimeondolewa. Dhambi zako zimeondolewa unapobatizwa; umekwisha kuziungama, na unaamini. Mbona usishike ile Kamba ya Kuokolea sasa inapopitia moyoni mwako, akisema, "Njoo upande huu, msafiri. Safiri pamoja Nami, jitwikeni msalaba Wangu. Jifunzeni Kwangu, kwa kuwa Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, na mizigo Yangu ni miepesi." Hebu nyosha mkono uishike.

138 Ni Wakristo wangapi walio Njiani usiku huu, ndani humu, ambao wana furaha kuwa walianza wakati mrefu uliopita? Umekwisha anza tayari na kote njiani, ungali unaelekea mwisho. Naomba kuwa Mungu ataivisha taji huduma yako, hata iwe ipi. Huenda ikawa ni bibi nyumbani. Naomba kuwa Mungu ataivisha taji huduma yako. Huenda ikawa ni mhubiri. Huenda ikawa ni shemasi. Huenda ikawa ni mkulima. Sijui ni nini. Cho chote ulicho, na Mungu na avishe taji maisha yako kwa utukufu wa Neno Lake, katika Kuja Kwake kwa pili akunyakue na akuchukue hadi Nchi nyingine ambako utajisikia tu kama samaki mdogo niliyenena habari zake, toka gizani mle chini. Unaona, hungeweza kuja kule juu ukiwa na mwili wa namna hii. Wala hungeenda juu kama wanaanga hawa, waona, yakupasa uwe katika pipa lililotiwa pumzi. Hujatiwa pumzi kwa ajili hiyo. Lakini Mungu akugeuzapo, umetiwa pumzi wakati huo, utakwenda katika kunyakuliwa basi. Wakati hisi hizi za kale za kidunia zimepotea, na umeenenda katika njia hiyo ya utukufu ya msalaba, ukienda Nyumbani pamoja na Yesu.

139 Sasa, Baba Mungu, twakushukuru kwa ajili ya mikono hii iliyoinuliwa juu ili wawe Wakristo. Naamini kuwa wao walilikusudia hivyo moyoni mwao. Nawaombea, kuwa hawatashindwa kwa wakati wo wote. Na wakishindwa, na upesi wampate yule mwombezi kwa Baba. Ambaye nimeona kuwa ni jambo kuu sana, Baba, hata ninapofanya makosa yangu yote, ndipo naona kuwa nina mwombezi (upesi sana) kwa Baba, katika Yesu Kristo. Nami narudishwa tena katika neema. Ule mkono wa upendo wa Bwana hufutilia mbali, na kunayo sadaka iliyojawa na damu pale ambayo naikiri kuwa Mwokozi wangu.

140 Wale wote walio wagonjwa, naomba kuwa utawapa mahitaji yao na uponye maradhi yote, Bwana. Nao walio hapa sasa wameketi chini ya upako huu wa utukufu wa Roho Mtakatifu, tunaposikia kwa utamu ukimwagwa juu ya nafsi zetu.

141 Baba Mungu, wajua lile nililokuwa nikiwaza nikija toka huko Canada hivi majuzi. Niliwazia, "Lo, jinsi ningependa kupata mkutano wa ufufuo wa mtindo wa kale tena, kuwaona wa—watakatifu wa Mungu wa—wakiimba na nguvu za Mungu zikishuka." Lo, jinsi moyo wangu utarajiavyo hayo, Bwana. Na kuzuke mkutano wa ufufuo Maskanini humu, lo, nguvu za Mungu zipate ku—kumwagwa katika vijito vya neema, ziingie kila moyo.

142 Nakushukuru kwa mahali hapa padogo, Bwana. Hatukuweza kupaweka hivi, imekuwa ni neema Yako iliyopaweka pa kiroho. Na sasa naamini, Bwana, mahali padogo palipo pa kiroho sana nchini, nipajuapo, ni papa hapa katika Njia ya Nane na ya Penn. Jinsi ninavyokushukuru kwa ajili ya hili Bwana! Kwenda makanisani na kuyaona yamepoa na yasiyojali, na wanawake wakavu wa macho hata hawana haya, na hakuna hata "amina" moja wala chozi shavuni mwao, wala cho chote, wala hamna wokovu, wala cho chote ila kujiunga tu na kanisa na kukariri kanuni zao za imani. Na, Ee Mungu, ndipo wanakuja mahali pazuri palipo na joto ambapo mioto imewashwa katika kila madhabahu ya moyo. Ni faraja jinsi gani, Baba! Ni faraja jinsi gani! Asante, Ewe Baba, na idumu hadi kuja kwa Bwana Yesu. Tubariki pamoja sasa.

143 Na kesho ni Sabato. Na, Bwana, nisaidie asubuhi, ikiwa itakuwa kura yangu kuhubiri juu ya kule *Kuhesabu Kinyumenyume*. Mungu, na niweze kukuhubiri katika njia fulani hata watu wakufahamu, Bwana. Na sasa na wao waone ile hali ya huduma, na kiwango ilichofikia, na kile tunachongoja, na kwa nini kila kitu kinaendelea jinsi kilivyo. Na wao wasome toka kifungu cha tano na kuendelea, ndiposa watambue mahali tunaposimama.

144 Na sasa, Baba, naomba kuwa utatubariki na kutupa pumziko nzuri miilini mwetu, na kuturudisha tena kesho. Wabariki watu hawa wote wanaosimama kote karibu na kuta,

na wakiegemea kwa mguu mmoja kisha mwingine. Wanawake, wanaume wamesimama huko nje, kwenye mvua, na karibu na madirisha, na wameketi magarini mwao. Na, wote wamesimama na . . . nami naomba kuwa utawabariki, Bwana. Na wao waende nyumbani wakiwa na neema ya Mungu mioyoni mwao. Naomba katika Jina la Yesu. Amina.

145 Je, mwafahamu sasa? Someni katika, kwanza, II Timotheo 2:4, II Timotheo 4, kuanzia kile kifungu cha 5 na kuendelea, kabla hamjalala usiku huu, mkiweza, nanyi mtaona tulipo. Mbona watu hao wakamwacha? Mbona yeye alikuja . . . Na sasa hebu linganisha huduma hiyo na ile tuliyo nayo leo. Linganisha na mafundisho ya Mtakatifu Paulo. Kumbuka katika kile kitu cha Kimbinguni nilichokiona, nilisema, "Vema, Paulo atapaswa kusimama na watu wake?"

Wao walisema, "Naam."

146 Nilisema, "Nimehubiri Neno lile lile yeye alilohubiri, nikadumu vivyo hivyo hasa na Injili ile ile."

147 Na mamilioni wakainua mikono yao na kusema, "Tunategemea hilo."

148 Bwana awabariki ni. Je, mwampenda? "Hata twonane huko juu! Hata twonane kwake kwema!"

Kiwango Cha Sasa Cha Huduma Yangu SWA62-0908
(Present Stage Of My Ministry)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi jioni, Septemba 8, 1962, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2017 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org